# Nipashe

Jumatatu Februari 25, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579850

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Baba afurahia mwanawe kufungwa kwa miaka 30

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**SIRRO: MAUAJI YA WATOTO YATAGHARIMU FEDHA NYINGI**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, amesema kuwa mauaji ya watoto yaliyotokea nchini yataigharimu serikali...

UKURASA WA 4

**DED AINGIA MATATANI MBELE YA WAZIRI MKUU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemnyooshea kidole Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Valerian Juwal, kwa kushindwa...

UKURASA WA 5

**CUF MAALIM SEIF KWENDA KWA CAG**

WAKATI uamuzi wa Mahakama kuhusu hatima ya uenyekiti wa Profesa Ibrahimu Lipumba katika Chama cha Wananchi (CUF), ukisubiriwa kwa hamu na wadau mbalimbali...



# Vifo 25, ajali 7, miezi 9 magari serikali

**NYINGINE** yaua 9 gari likitumbukia mtoni...

*Endelea ukurasa wa 2*

Gari aina ya Toyota Land Cruiser Hard Top mali ya Taasisi ya Uhifadhi wa Wanyamapori (TAWA), lililokosa mwelekeo na kutumbukia katika Mto Kikwalila Ifakara wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro na kusababisha vifo vya watumishi 9 wa Mradi wa Kuwezesha Upimaji na Urasimishaji wa Ardhi ulio chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Ndoo 226 zanaswa sampuli dhahabu

UKURASA 2

# Kiama waliojimilikisha mali za NMC chakaribia

UKURASA 2

MICHEZO USIYOYAJUA SIMBA VS AZAM FC TAIFA UK. 15 MAONI, KATUNI UK.6

# Ndoo 226 zakamatwa na sampuli 883 za dhahabu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza inalishikilia gari aina ya Fuso lenye namba ya usajiri T 906 AGB lililonaswa wilayani Sengerema likiwa linasafirisha ndoo 226 zenye sampuli za madini 883.

Imedaiwa kuwa, sampuli hizo ni mali ya Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) zilizokuwa zikitoka mkoani Geita kwenda Mwanza.

Gari hilo lilikamatwa juzi alfariji na askari waliokuwa doria baada ya kubaini shehena iliyokuwamo ndani ya gari iliyokuwa ikipelekwa maabara ya kupima sampuli za madini ya SGS iliyoko jijini Mwanza, ilikuwa na upungufu wa vibali vinavyoruhusu mzigo kusafirishwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alidai kuwa baada ya askari kulikamata gari hilo, walikuta ndoo 226 zikiwa hazina kibali cha serikali kinachoonyesha uhalali wa usafirishwaji wake.

"Vyombo husika naagiza mfanye uchunguzi wa kina kuhusu jambo hili ili uhalali wa shehena ya mzigo huu uweze kubainika, maana maelezo ya Ofisa Madini Mkazi wa GGM, Gasper Kachenge, hayajitoshelezi, anadai mzigo unaozunguka ndani ya nchi hauhitaji kibali, jambo ambalo haliwezekani," Mongella alidai.

Mkuu wa Mkoa huyo alidai kuwa kwa mujibu wa taratibu za kazi, ni lazima kila hatua iwe na maelezo ya maandishi na siyo kujiridhisha kwa macho tu kama ilivyoelezwa na Kachenge.

Alidai atatumia wataalamu wa Sheria ya Madini akiwamo Kamishina wa Madini, kutoa ufafanuzi zaidi juu sheria na utaratibu wa usafirishaji madini kutoka eneo moja kwenda lingine ikibainika kuna ukiukwaji wowote wa sheria, hatua stahiki zitachukuliwa.

Ofisa Madini Mkazi wa GGM, Kachenge, alipoulizwa na Mongella sababu za shehena hiyo kusafirishwa hadi jijini Mwanza kwa ajili ya vipimo licha ya maabara husika kuwapo mgodini, alidai:

"Vielelezo vya mzigo huu vipo ila nilichelewa kuvisaini maana mzigo ulitakiwa kutoka tarehe 21 mwezi huu, lakini kutokana na majukumu mengi niliyo nayo, nilichelewa kuandaa kibali.

"Kuna stakabadhi hizo zilizoandikwa tarehe 22, mwezi huu, lakini sheria haisemi wazi mzigo unaokuwa ndani ya nchi kama unatakiwa kuwa na vibali isipokuwa unaotoka nje ya nchi."

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Sengerema, Bena Msoma, alidai kuwa baada ya kulikagua gari hilo na kukuta shehena hiyo, waliagiza kuonyeshwa vibali vinavyoonyesha uhalali wa usafirishaji wa mzigo huo, walipewa kimoja kilichotolewa na GGM.

"Mzigo huu tumebaini unasafirishwa kinyume cha utaratibu unaoelekezwa na sheria husika, tulimuuliza ofisa wa madini mgodini (Kachenge), aliutambua lakini hakukuwa na vibali vya serikali na alitujibu tu kwa mdomo pasipo na vielelezo," Msoma alisema.

# Vifo 25, ajali 7, miezi 9 magari ya serikali

**Na Waandishi Wetu**

WATAALAMU tisa wa Programu ya Kuwezesha Upimaji na Urasimishaji wa Ardhi (LTSP), wamefariki dunia na wanne kunusurika, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kutumbukia mtoni.

Taarifa ya Jeshi la Polisi ilisema ajali hiyo ilitokea juzi jioni Ifakara wilayani Kilombero baada ya gari kuacha njia, kuanguka na kuzama ndani ya Mto Kikwawila.

Kufariki dunia kwa maofisa hao, kunafanya idadi ya vifo vya watumishi serikalini kutokana na ajali za barabarani kufika 25, ikiwa ni ajali ya saba katika kipindi cha miezi tisa hadi sasa, nyingi zikitawaliwa na magari mwendokasi, kuacha njia na kupinduka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa gari lililobeba wataalamu wa programu hiyo iliyoko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema gari hilo ni lenye namba za usajili STK 9444 aina ya Toyota Landcruiser Hard Top, mali ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa).

Kamanda Mutafungwa alisema gari hilo lilikuwa linaendeshwa na Baraka Zefrini ambaye ni miongoni mwa walionusurika katika ajali hiyo.

Alibainisha kuwa, baada ya taarifa za kitabibu kuonyesha hakuwa amejeruhiwa, Jeshi la Polisi lilimkamata dereva huyo na anatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya uchunguzi wa ajali kukamilika.

"Dereva alikuwa katika mwendokasi, akashindwa kumudu gari na kugonga kushoto mwa daraja na kutumbukia mtoni na kusababisha vifo vya watu tisa papohapo, huku wanne wakinusurika," Kamanda Mutafungwa alisema.

Aliongeza kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 11 kwenye eneo hilo la Kikwawila katika mji mdogo wa Ifakara.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Festus Ponela, alisema waliliona gari hilo likishuka kwa kasi katika mteremko jirani na mto huo na baadaye kuingia mtoni.

Alisema wananchi wanaoishi jirani na eneo la tukio, walijitokeza kusaidia kuopoa miili ya waliofariki dunia na kuwaokoa majeruhi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, James Ihunyo, alisema waliofariki dunia ni wanaume watano na wanawake wanne.

Ihunyo alisema gari hilo lilikuwa linatumiwa na wataalamu hao katika upimaji na ugawaji wa hati za ardhi katika vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Kilombero kupitia LTSP.

Alisema programu hiyo ni ya miaka mitatu na kwa sasa iko katika majaribio ya utekelezaji kwenye

INAENDELEA UK. 8



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Ewura Kanda ya Kaskazini, Injinia Lorivii Long'du, akizungumza na watendaji kata kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga, wakati wa semina elekezi kwa watendaji hao. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Kiama chaja waliojimilikisha mali NMC

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imedhihirisha kusudi lake la kuwabaini na kuwanasa waliojinufaisha na kujimilikisha mali za Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) kwa kutangaza kikosi kazi.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ndiye aliyekitangaza kikosi kazi hicho kinachounda kamati ya kuhakiki mali za Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko zilizokuwa zikimilikiwa na NMC.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa katika matangazo kwenye vyombo vya habari na wizara hiyo, kamati hiyo ambayo imepewa hadidu za rejea ikamilishe kazi hiyo ndani ya siku 30 tangu ilipoteuliwa.

Kamati hiyo iliyoteuliwa na Waziri Hasunga tangu Februari 11, mwaka huu, na inaundwa na watu watano.

Majina ya wajumbe hao ni Asangye Bangu ambaye ndiye mwenyekiti. Mengine ni Hangi Chan'ga, Sande Mnozya, Tabea Ndibalema na Paul Chacha.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu hatua hiyo, Waziri Hasunga alifafanua kwa kifupi kwamba kuna mali zilikabidhiwa bodi, lakini hazipo.

Alitoa agizo hilo alipokuwa akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Awali Septemba 21, mwaka 2017 aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Charles Tizeba, alitangaza nia ya kufanya uhakiki wa mali hizo.

Alisema mali zote za NMC ambazo hazikuuzwa zitamilikiwa na bodi hiyo, huku akiwataka kuingia upya mikataba na kuisimamia ili kuondoa ubabaishaji wa baadhi ya watu waliojimilikisha mali za serikali.

Naye Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Kijaji, akijibu swali hilo bungeni, alisema katika kubinafsisha mali za NMC, serikali imepata Sh. bilioni 7.4.

Kijaji alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Liwale, Mohamed Kuchauka, ambaye alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha zilizopatikana katika kubinafsisha mashirika hayo.

Alihoji kuwa NMC lilikuwa na matawi karibu nchi nzima na mali mbalimbali na lilibinafsishwa kutokana na sera ya ubinafsishaji, ni matawi mangapi yamebinafsishwa na mangapi yamebaki mikononi mwa serikali.

Serikali ilibinafsisha matawi 22 ya shirika hilo la NMC ambapo ilijipatia Sh. bilioni 7.4 na matawi matano imebaki nayo.

Miongoni mwa mali zilizokuwa zikimilikiwa na shirika hilo ni pamoja na vinu na mashine mbalimbali za usagishaji wa nafaka.

HABARI KITAIFA



Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, Amina Mollel, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Oldonyowas, Wilaya ya Arumeru mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba afurahia mwanawe kufungwa jela miaka 30

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MZEE Musa Katambo, baba mzazi wa Ally Katambo (30), ambaye amehukumiwa kwenda jela miaka 30 baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara kumkuta na hatia ya kumbaka mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 11, amefurahia kifungo cha mwanawe.

Ally alitiwa hatiani na kupewa adhabu hiyo kutokana na kumfanyia binti yake huyo mwanafunzi wa darasa la nne kitendo cha kinyama.

Mzee huyo alishangilia na kuipongeza mahakama kwa kutoa hukumu hiyo ya kifungo cha miaka 30 jela dhidi ya mwanae, akisema kosa alilolifanya la ubakaji ni kinyume cha sheria za nchi.

Katambo ambaye anaishi kijijini kwake Ndanda wilayani Masasi Mkoani Mtwara, alisema kwamba hajutii maamuzi ya mahakama dhidi ya mtoto wake huyo kufungwa miaka 30 jela, na kwamba serikali imetenda haki katika kusimamia sheria hasa juu ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mzee Katambo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na gazeti hili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Masasi, baada ya mtoto wake huyo kuuhukumiwa kwenda jela miaka 30.

Alisema amefurahishwa na hukumu hiyo kwa sababu itatoa fundisho kwa vijana wengine wenye tabia kama ya mtoto wake kwa kuwa watakaposikia wataacha kufanya vitendo hivyo, ambavyo vinaonekana kuchochewa na imani za kishirikina, badala yake vijana wafanye kazi kwa bidii ili waweze kutimiza ndoto zao.

Alisema serikali ya sasa inasimamia haki kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto

INAENDELEA UK. 8

## Sirro: Mauaji ya watoto yatagharimu fedha nyingi

**Na Salome Kitomari**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, amesema kuwa mauaji ya watoto yaliyotokea nchini yataigharimu serikali fedha nyingi.

IGP Sirro alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza na kamati za ulinzi na usalama za wilaya ya Kwimba na Magu, mkoani Mwanza katika operesheni ya kuwahoji waganga wa kienyeji katika mikoa ya Mwanza, Simiyu na Geita.

"Viongozi wa dini wachukue nafasi yao kuelewesha wananchi hasa waganga wakienyeji, wamuogope Mungu, wafuate sheria na wasifanye ramli chonganishi ambayo mwisho wa siku inasababisha mauaji," alisema na kuongeza:

"Mtu mmoja akifa kwa sababu ya ramli chonganishi inagharimu serikali fedha nyingi sana, kwa mfano mauaji yaliyotokea Simiyu, fedha nyingi ya serikali itatumika maana tumetuma wapelelezi, magari yatafanyakazi, mimi (IGP) nitakwenda na viongozi wengi watakwenda, hivyo lazima mtu mmoja anayeleta matatizo wananchi tumbaini na kumshughulikia mapema,"

INAENDELEA UK. 8

# Majaliwa azungumzia utekelezaji ahadi za JPM

**Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewahakikishia wananchi kwamba ahadi zote zilizotolewa na Rais John Magufuli katika maeneo mbalimbali nchini, zitakuwa zimetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 90 ifikapo mwaka 2020.

Pia Waziri Mkuu amesema serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuwahudumia wananchi na kuhakikisha huduma mbalimbali za kijamii kama maji, afya, nishati, elimu na miundombinu zinapatikana kwa uhakika.

Alitoa kauli hiyo Jumamosi jioni alipozungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Kituo cha Polisi cha Tarakea wilayani Rombo, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kilimanjaro.

Waziri Mkuu alisema wananchi waendelee kuwa na serikali yao ambayo imejipanga kutekeleza ahadi zote zilizotolewa na Rais Magufuli kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020 inavyoelekeza.

Aidha, Waziri Mkuu, alisema mtumishi mzembe, mwizi, mla rushwa na asiyewajibika hana nafasi katika serikali ya awamu ya tano, hivyo kutoa wito kwa watumishi wote waimarishe utendaji wao.

Waziri Mkuu alisema kila mtumishi wa umma anatakiwa kuhakikishe anafanya kazi kwa bidii, ili kuiwezesha serikali kutimiza lengo lake la kuboresha maendeleo ya wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini hususan ya vijijini.

"Iwapo watumishi wa umma watatimiza majukumu yao ipasavyo, changamoto nyingi zinazowakabili wananchi kama upatikanaji wa maji zitakuwa historia kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo."

Waziri Mkuu alisema kwa sasa serikali inatekeleza kampeni ya Rais Magufuli ya kumtua mama ndoo kichwani, ambapo itahakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma ya maji karibu na makazi yao.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu jana, aliweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa maabara ya afya ya jamii kwenye Hospitali ya Taifa ya magonjwa ambukizi ya Kibong'oto na kusema kuwa amefarijika kuona lengo la Rais Magufuli katika sekta ya afya likitekelezwa.

Alisema Rais Magufuli anataka kuona Watanzania wote wanapata huduma mbalimbali za kijamii.

Waziri Mkuu alisema hayo alipotembelea hospitali hiyo ya Kibong'oto iliyoko kwenye Mtaa wa Mae Kata ya Ivaeny, wilayani Siha.

"Rais wetu Magufuli ana nia thabiti ya kuwahudumia Watanzania wote walioko katika

INAENDELEA UK. 8




# DED aingia matatani mbele ya Waziri Mkuu

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemnyooshea kidole Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Valerian Juwal, kwa kushindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Imeelezwa kuwa hadi sasa, mkurugenzi huyo amefanikiwa kukusanya mapato ya mwaka huu wa fedha kwa asilimia 38 ya lengo.

Vilevile, Majaliwa ameeleza kukerwa na safari za mara kwa mara zisizo na tija za mkurugenzi huyo na kumtaka kuachana na safari hizo ambazo aliweka wazi kuwa hajaagizwa na serikali.

Waziri Mkuu alimweleza hayo mkurugenzi huyo jana, alipozungumza na watumishi wa Halmashauri ya Siha katika mji mdogo wa Sanya Juu.

"Nimesikia taarifa ya Mkuu wa Wilaya (Onesmo Buswelu) akisema kwamba, hajaridhishwa na kasi ya ukusanyaji wa mapato. Ni kweli. Kwanini hamjafikia asilimia 50, leo ni Februari?

"Na wewe mkurugenzi, Morogoro unaenda wewe, Dodoma unaenda wewe, Dar es Salaam unaenda wewe. Wape fursa ya kwenda kule pia unakokwenda. Baada ya maelezo haya, sitarajii mgongano kati ya madiwani na watendaji," Majaliwa alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, mkurugenzi huyo hafuatilii shughuli za halmashauri na moja ni miongoni mwa maofisa wanaoondoka mara kwa mara kwenye kituo cha kazi.

Alipoitwa na Waziri Mkuu kueleza kwanini hawajafikia hata asilimia 50 ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, Juwal alisema: "Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika mpango ule ambao ni chanzo cha mazao, hatukufanikiwa kukusanya kutokana na hali ya hewa, lakini kiwango kilichobajetiwa kilikuwa kikubwa kwenye mazao na ardhi."

Mkurugenzi huyo pia alionywa na kupewa muda usiojulikana kujirekebisha, kinyume chake, serikali haitasita kuchukua hatua za kinidhamu dhidi yake.

"Haiwezekani ukawa wewe mkurugenzi unajichukulia uamuzi wa kwenda nje ya mkoa bila kibali cha katibu tawala wa mkoa... kwa mwenendo huo, ni wakati gani mtapanga mipango ya maendeleo ama kukusanya mapato ya ndani?" Waziri Mkuu alihoji.

Kiongozi huyo wa serikali pia aliiagiza halmashauri hiyo kuhakikisha inafikia kiwango cha asilimia 80 katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Mkuu Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema changamoto kubwa inayoikabili wilaya hiyo ni kuwapo kwa migogoro mingi ya ardhi ukiwamo wa mpaka wa Arumeru na Siha.

*Celebrating a Beautiful Life of*

*David Robert Mareale*



15 June 1933 – 25 February 2014

**Jeremiah 29:11;**

*"For I know the plans I have for you," declares the LORD, "plans to prosper you and not to harm you, plans to give you hope and a future."*

*February 25th, 2019 We celebrate your 5th anniversary since you departed from us, your absence has always been felt in our lives as we reminiscence beautiful memories shared and always treasured. On this day, We thank God for your life which we were blessed and privileged to share with you and the love displayed to us in ways that you raised us and loved Mum. Lord, We give thanks for the life you gave our Dad and the teaching impartations we received through him as you worked through his life. We thank our Father for allowing God to do so and hence receiving the blessings that unlocked this generation.*

*Your life was a blessing, your memory a treasure*
*We love you beyond words, and miss you beyond measure*
*The teachings you instilled in us, we will forever treasure*
*A life well lived who can tell, but God alone can truly measure.*

*Your Undeniable* **Legacy** *still lives Forever!*

*Remembered by your loving Wife – Mary, your Children – Regina, Stella, Zaituni, Nderima, Ngianasia, Kindondechi, Makyalen and Makicha, your Son-in-law – Brigadier Reginald Chonjo, Leonard Masonu and David Minja; and your lovely Grandchildren Mbenda, Irene, Karen, George, William, Joshua, Exter, Louis David and Robert, without forgetting all other Members of the Family, Relatives and Friends who loved you dearly.*

**The Dar es Salaam 2016-2036 Master plan (DMP)**

**YAH: MAANDALIZI YA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA DAR ES SALAAM 2016 - 2036**

**MAONESHO YA HADHARA (26-28 Februari 2019)**

Tunapenda kuwaalika kwenye Maonesho ya Hadhara ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam itakayofanyika Makumbusho ya Taifa, kuanzia tarehe 26 – 28 Februari 2019 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:

| Na. | Tarehe | Mawasilisho ya 1 | Mawasilisho ya 2 | Kiongozi Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 26.2.19 | 5 asubuhi | 9 Alasiri | Dr. C. T. Lekule |
| 2. | 27.2.19 | 5 asubuhi | 9 Alasiri | Dr N. Mushi |
| 3. | 28.2.19 | 5 asubuhi | 9 Alasiri | Mr John Lubuva |

Tumepanga mahudhurio maalumu ya wajumbe kutoka kwenye Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kuanzia saa 9 alasiri mnamo tarehe 26 Februari 2019 saa 9 alasiri, Bodi ya Usajili wa Maafisa wa Mipango Miji kuanzia saa 9 alasiri mnamo tarehe 27 Februari 2019 na Bodi ya Usajili ya Wahandisi kuanzia saa 9 alasiri mnamo tarehe 28 Februari 2019 kwaajili ya mawasilisho Maalumu na mjadala katika hayo maeneo husika.

Haya Maonesho ya Hadhara yatakuwa huru kwa kila mtu na muda wakuingia na kutoka utakuwa sambamba na utaratibu muda wa kuingia na kufunga wa jingo la Makumbusho ya taifa.

Wenu Mtiifu,

.......................... (+255754272417)

**Dr. C.T. Lekule**
**Mtaalamu Kiongozi Muelekezi na Muwakilishi wa Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam.**



Mtaalamu wa Tiba Radiolojia (Interventional Radiology) wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Erick Mbuguje (kulia), akitoa usaha kwenye jipu lililoko ndani ya ini la mgonjwa, huku akiongozwa na Dk. Troy Koch kutoka Chuo Kikuu cha Utah, Marekani. **MPIGAPICHA WETU**

# Makumbusho ya kisasa ya sokwe mtu kujengwa

**Novatus Makunga,** ARUSHA

TAASISI ya Kimataifa ya Jane Goodall, imeanza ujenzi wa makumbusho maalum ya sokwe mtu jijini Arusha yatakayokuwa na teknolojia ya kisasa zaidi inayoendana na ulimwengu, yakiwa ya kwanza kujengwa duniani.

Akizungumza wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi huo jana, mwasisi na mwenyekiti wa taasisi hiyo, Dk. Jane Goodall, alisema kujengwa kwa makumbusho haya jijini hapa ni kutokana na muhimu wake kwa Watanzania na wageni wa kimataifa watakaotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini.

Dk. Jane Goodall alieleza kuwa watalii watakaotembelea vivutio mbalimbali vya utalii wakiwamo Watanzania wenyewe watatumia kituo cha makumbusho haya kupata elimu juu ya umuhimu wa masuala ya uhifadhi wa maliasili, uhifadhi wa mazingira na wanyamapori.

"Makumbusho haya hayatatumika kwa ajili ya watafiti, wanasayansi, wanafunzi pekee bali yamejengwa kwa faida ya jamii mbalimbali duniani," alisisitiza.

Alisema kituo hicho kitatumika kuwaunganisha vijana katika kujitolea na pia kuonyesha kazi mbalimbali zinazofanywa na Taasisi mbalimbali katika suala zima la uhifadhi.

Alifafanua kwamba amekuwa akialikwa sehemu mbalimbali duniani kuzungumza na wanafunzi na waumini katika nyumba za ibada kuhusiana na uhusiano wa moja kwa moja kati ya imani na huruma kwa viumbe wote wakiwamo wanyama na binadamu.

Kwa mujibu wa utafiti wa Dk. Goodall, sokwe anamkaribia binadamu kwa zaidi ya asilimia 90 ambapo pia utafiti wake unabainisha kwamba mahala anapolala sokwe ni bora zaidi kuliko malazi ya binadamu.

Mwenyekiti Mwenza wa taasisi hiyo, James Lembeli, alisema makumbusho hayo ni dhamana kubwa iliyotolewa na taasisi hiyo kwa Watanzania katika suala zima la uhifadhi.

"Makumbusho haya yatatoa taswira halisi juu ya dira ya masuala ya uhifadhi na umuhimu wake kwa dunia nzima ambapo pia katika makumbusho haya utapatikana utafiti uliofanywa na Dk. Goodall na machapisho yake kwa faida ya dunia nzima," alisema Lembeli.

Lembeli ambaye aliwahi kuwa mwenyekiti wa kamati ya bunge ya Maliasili,Ardhi na Mazingira, alisema Dk. Jane Goodall kwa zaidi ya miaka 60 ametumia muda wake mwingi kufanya utafiti kuhusu masuala ya maisha, tabia na mwenendo wa sokwe mtu. Alisema wakati akianza shughuli za utafiti wa sokwe katika hifadhi ya Gombe ilikuwa vigumu sana sokwe hao kumkaribia kutokana na kumwogopa mtu mweupe.

Lembeli alisisitiza umuhimu kwa vijana kutumia taasisi hiyo kuendeleza shughuli za utafiti na uhifadhi ambapo mtafiti huyo taasisi yake imetilia mkazo mipango bora ya matumizi ya ardhi.

Lembeli alisema makumbusho hayo ni ya kwanza kujengwa na taasisi hiyo duniani ambapo alisisitiza umuhimu wa Serikali ya Tanzania kutambua umuhimu wa mtafiti Dk. Jane Goodall katika suala la uhifadhi, matumizi bora ya ardhi na mchango wake katika masuala yote ya uhifadhi.

Makumbusho hayo yanatarajia kukamilika mwakani wakati taasisi hiyo itakapokuwa ikiadhimisha miaka 60 tangu Dk. Jane Goodall aanze shughuli za utafiti wa sokwe katika Hifadhi ya Taifa Gombe.

Naye, mtafiti Anthoony Tonny wa taasisi hiyo, alisema inakadiriwa kuwa Tanzania bado ina sokwe kati ya 1,700 na 2,300 ambapo Taasisi, na kwamba taasisi hiyo inafanya kazi na nchi zaidi ya 30 duniani.

Dkt Jane Goodall, ambaye ni Raia wa Uingereza, alianza shughuli za utafiti rasmi katika muala ya sokwe katika hifadhi ya Gombe miaka ya 1960 akiwa na umri wa miaka 26, na hivi sasa ana umri wa miaka 86

Ujenzi wa makumbusho haya yatakayogharimu zaidi ya shilingi bilioni moja, unafanyika katika eneo la Cultural Heritage, baada ya mmiliki wa eneo hilo, Saifudin Khanbhai, kutoa bure sehemu ya ardhi.

Mbali na ujenzi wa makumbusho hayo, taasisi ya Jane Goodall imetoa zaidi ya shilingi bilioni 45 katika miradi mbalimbali hususan ya uhifadhi wa misitu ya asili, matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa sokwe.

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa tatu kutoka kulia), akiwa katika machimbo ya Nyakafuru yaliyoko katika Kijiji cha Nyakafuru wilayani Mbogwe mkaoni Geita, ambapo aliwaahidi wachimbaji wadogo wa eneo hilo kupata umeme ndani ya siku kumi. **PICHA: TERESIA MHAGAMA**

## CUF Maalim Seif wajipanga kwenda kwa CAG

**Na Enock Charles**

WAKATI uamuzi wa Mahakama kuhusu hatima ya uenyekiti wa Profesa Ibrahimu Lipumba katika Chama cha Wananchi (CUF) ukisubiriwa kwa hamu na wadau mbalimbali wa siasa, chama hicho upande wa Katibu Mkuu, Maalim Seif Sharif umekusudia kupeleka barua kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ili kukagua mahesabu ya chama hicho.

Jumanne iliyopita Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilitengua uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wadhamini ya chama hicho walioteuliwa na kambi ya Prof. Lipumba na kusajiliwa na Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (Rita). Maalim Seif Sharif Hamad akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za wabunge wa CUF Magomeni , Dar es Salaam baada ya uamuzi huo alimtaka AG, Prof. Mussa Assad, kufanya ukaguzi wa fedha za ruzuku za chama hicho.

Tayari Prof. Mussa Assad ameshaonyesha nia ya kufanya ukaguzi iwapo atapewa taarifa rasmi kutoka katika chama hicho.

Akikaririwa na gazeti moja la kila siku nchini, Prof. Assad alisema bado hajapewa taarifa rasmi ya kufanya ukaguzi na akipewa taarifa hiyo ataiangalia kwanza.

"Siwezi kusema lolote kwa sasa, lakini ikija taarifa official (rasmi) nitaiangalia kwanza," Prof. Assad alisema.

Akizungumza na gazeti hili jana, Naibu Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa chama hicho upande wa Maalim Seif , Mbarala Maharagande, amedai kuwa wataamua suala hilo baada ya kufanya vikao vya chama.

"Tutaamua baada ya vikao na tutatoa taarifa, kwa sasa tunafuatilia namna ya kukirejesha chama katika mikono salama," Maharagande alisema.

Tangu kurejea kwa Prof. Lipumba kama mwenyekiti wa chama hicho kumekuwapo na migawanyiko na mivutano baina ya viongozi na wanachama wa chama hicho, jambo lililosababisha hata baadhi ya wabunge wa chama hicho kujiuzulu na wengine kutenguliwa ubunge wao baada ya mwenyekiti huyo kuteua wabunge wapya.

Ijumaa iliyopita Mahakama Kuu iliahirisha kutoa hukumu ya kuamua iwapo Prof. Lipumba ni mwenyekiti halali wa CUF ama la na kutangaza kusogeza mbele hukumu hiyo hadi Machi 17, mwaka huu kwa maelezo kuwa Jaji Dk. Benhajj Masoud amepangiwa majukumu mengine nje ya ofisi.

## Mnada mkubwa wa dhahabu rasmi

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WAFANYABIASHARA wa madini ya dhahabu 127 wakiwamo 13 wamepewa leseni kubwa na wengine 114 za kawaida, ikiwa ni shehemu ya utekelezaji wa maandalizi ya kufunguliwa kwa mnada mkubwa wa dhahabu mkoani hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alisema hayo jana wakati akikagua kazi ya maandalizi ya ujenzi wa vyumba maalum kwa ajli ya taasisi za fedha na wanunuzi wakubwa na wa kawaida unaoafanyika katika jengo la kituo cha biashara mjini Geita.

Gabriel alisema mnada huo utafunguliwa wakati wowote kuanzia sasa baada ya mahitaji yote yaliyobakia kukamilika huku kazi ya ujenzi na marekebisho ikifanyika usiku na mchana.

Baadhi ya taasisi za fedha zilizoko katika hatua ya mwisho ya kukamilisha maandalizi ya kushiriki katika utoaji huduma za mnada huo wa dhahabu ni Azania na CRDB, na kwa mujibu wa utaratibu huo, Mkoa wa Geita utakuwa na vituo vinne vya kununulia dhahabu kikiwamo cha makao makuu Geita Mjini.

Kuhusu suala la ulinzi na usalama katika mnada huo mkubwa wa dhahabu nchini, alisema utawekwa mfumo wa kisasa wa ulinzi na usalama ikiwamo kamera maalum na kuwapo askari polisi maalum.

Paulo Maliganya, Maduhu Mubarak na Hussein Mwananyanzala, miongoni mwa waliopewa leseni za ununuzi wa dhahabu, walipongeza serkali kwa kusikia kilio chao wakisema utawapunguzia kero na hofu ya kukamatwa kamatwa.

## Wadau wa siasa walilia mikutano

**Na Enock Charles**

IKIWA imebaki miezi michache kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa na pia mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu, wadau wa siasa wamezungumzia mikutano ya hadhara wakitaka iruhusiwe ili kutoa fursa kwa vyama kukutana na wananchi.

Wakati Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikikanusha kufanya mikutano ya hadhara, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimeshatangaza kusudio la kufanya mikutano hiyo, licha ya kupigwa marufuku na serikali tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.

Naibu Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa Chama cha Wananchi (CUF), Mbarala Maharagande, amesema wanajiandaa kuja na uamuzi wa kutekeleza azimio la Arusha lililohusisha vyama vya Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambalo lilipingana na zuio la mikutano.

"Chama ni vikao, wenzetu wa Chadema wamekuja na uamuzi huo baada ya kikao na sisi tutakuja na maamuzi yetu, ingawa tulishatoa tamko la kupinga zuio hilo miaka mitatu iliyopita," Maharagande alisema.

Naye Katibu Mwenezi wa ACT-wazalendo, Ado Shaibu, amedai ni muhimu kwa chama kukutana na wananchi wake na njia sahihi ni kupitia mikutano ya hadhara, hivyo kuitaka serikali kuondoa zuio hilo kwa madai kuwa lipo kinyume cha sheria.

"Tutakaa vikao kuona 'how to operationalise' azimio letu la Zanzibar kwa sababu kutamka ni jambo moja na kutekeleza ni jambo lingine," Shaibu alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Ada-Tadea, John Shibuda, akizungumza na gazeti hili lililotaka kufahamu msimamo wake kuhusiana na mikutano ya hadhara, alidai kuwa anasubiri kupata uamuzi wa mwisho utakaofanyika kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Mimi bado naisubiri Sheria ya Vyama vya Siasa kwa sasa siwezi kuwa mpiga ramli katika giza kujua itasainiwa ama la baada ya hapo sasa nitaweza kutoa tamko," Shibuda alisema.

Alipoulizwa iwapo sheria hiyo itasainiwa na Rais uamuzi wa ama kusainiwa au kutosainiwa atachukua uamuzi gani, alidai atawasiliana na serikali ili kujua hatima ya zuio hilo.

"Nitawasiliana na serikali ili kujua hatima ya zuio la mikutano ya vyama vya siasa," aliongeza Shibuda.

Mkazi wa Mabibo jijini Dar es Salaam, Ezron Mollel, akitoa maoni yake kuhusiana na vyama kufanya mikutano ya hadhara, alidai kuwa ni vyema sasa serikali ikafikiria upya suala hilo kwa mustakabali mwema kwa taifa.

"Mikutano hii ilizuiwa kwa nia njema tu, lakini sasa kwa kuwa tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu upo karibu ni vyema vyama viachiwa vikutane na wanachama wao," Ezron alisema.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO

TAARIFA KWA UMMA

HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

24 FEBRUARI 2019

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawaomba radhi Wateja wake wa Mkoa wa Dar es salaam kwa kukosa huduma ya umeme kwa siku za hivi karibuni kutokana na maboresho makubwa yanayohusisha matengenezo kinga ya mashine 3 za Kituo cha Ubungo II, pamoja na uwekaji wa transfoma kubwa la MVA 300 kwenye Kituo cha kupoza umeme cha Ubungo ili kukiongezea uwezo na kwenda sambamba na ukuaji wa mahitaji ya jiji la Dar es Salaam.

Kabla ya matengenezo kuanza mnamo Januari 2019 Kituo hiki cha kupoza umeme cha Ubungo kimekuwa kinapokea umeme kutoka katika vituo vya Uzalishaji umeme vilivyopo upande wa msongo wa kilovolti 220 kupitia transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 150 kila moja, zenye kupokea umeme wa msongo wa Kilovolti 220 na kuushusha hadi kuwa msongo wa Kilovolti 132 katika transforma namba sita na namba saba za kituo cha Ubungo na vituo vya uzalishaji umeme vilivyoungwa kwenye msongo wa kilovolti 132 ambavyo vimeungwa moja kwa moja kwenye mfumo mkuu wa usambazaji umeme kwa Dar es Salaam na Zanzibar.

Kutokana na matengenezo yanayoendelea vituo vya uzalishaji umeme vilivyoungwa kwenye msongo wa kilovoti 132 na 33 vimekuwa nguzo kubwa ya upatikanaji wa umeme. Vituo hivyo ni Ubungo II na Tegeta.

Shirika kupitia wataalamu wake tayari limefanya jitihada kubwa za kupunguza athari za upungufu wa upatikanaji wa umeme kwa wakaazi wa Dar es salaam na Zanzibar kwa kufanya yafuatayo:

Mosi, Kufungua laini ya msongo wa kilovoti 132 kati ya Kilimanjaro na Hale: Hili hufanyika ili kutoruhusu umeme wa kutoka Dar es Salaam na Morogoro kwenda Kilimanjaro hivyo Mkoa huu kuchukulia kwenye upande wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Arusha.

Pili , Kuwezesha upatikanaji wa umeme katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dar es salaam, kwa kuunga baadhi ya njia za Usafirishaji umeme kutoka Kituo cha Kinyerezi, Gongolamboto hadi Mbagala ili kuwezesha maeneo hayo kupata umeme bila kupitia kituo cha Ubungo ambacho kipo katika matengenezo.

Tatu, Kufungua njia ya umeme ya kilovolti 132 itokayo Kituo cha Kunduchi hadi Mlandizi na kuunga maeneo hayo katika njia ya umeme ya kilovolti 132 itokayo Morogoro ili kuwezesha jiji la Dar es salaam kuwa na umeme wa uhakika.

Nne, Kufungua laini ya msongo wa kilovolti 132 kati ya Ubungo na Chalinze upande wa Ubungo ili kutozihusisha transfoma za Ubungo kwenye mzigo wa mikoa mingine na hivyo kutumika kuhudumia wateja wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee.

Tunatarajia matengenezo haya yanayokwenda kwa awamu yatakamilika ifikapo mwezi Juni 2019.

TANESCO itaendelea kutoa taarifa ya Maendeleo ya kazi ya matengenezo ya kituo cha Ubungo yenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika Dar es salaam na Zanzibar kwa siku zijazo.

Imetolewa na: Ofisi ya Uhusiano
TANESCO-Makao Makuu

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF sasa igeukie viwanja hivi kunusuru wachezaji

**LIGI** Kuu Tanzania Bara kwa sasa ipo katika mzunguko wa lala salama huku Yanga ikiwa kileleni na pointi 61 baada ya kushuka dimbani mara 25. Kati ya timu 20 zinazoshiriki kinyang'nyiro hicho msimu huu, ni Simba tu ambayo ipo nyuma michezo saba hii ikitokana na kukabiliwa na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, pamoja na changamoto nyingi zinazoikabili ligi hiyo ikiwamo kukosekana kwa mdhamini mkuu, pia ubovu wa viwanja hususan vya mikoani kwa upande wa eneo la kuchezea "pitch" limekuwa tatizo sugu ambalo linazidi kufumbiwa macho. Kwa ujumla viwanja rafiki kwa soka nchini havizidi sita kati ya vyote vinavyotumika katika ligi hiyo ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Ukiacha Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex (Chamazi) vilivyopo jijini Dar es Salaam viwanja vingine rafiki kwa soka ni vilivyopo mikoani ni Uwanja wa Nyamagana wa nyasi bandia unaotumiwa na Alliance FC (Mwanza) na ule wa CCM Kirumba ambao hutumiwa na Mbao FC.

Kadhalika, Uwanja wa Kaitaba (nyasi bandia) unaotumiwa na Kagera Sugar unakamilisha orodha ya viwanja sita vilivyo rafiki kwa soka nchini. Na vilivyobaki havina sifa kabisa ya kuendelea kutumika, hali ambayo ni hatari sana kwa maendeleo ya soka letu tunapotafuta mwakilishi mwenye sifa stahiki na aliyepatikana kihalali kuweza kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nipashe tunaamini kama Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kushirikiana na wizara husika ya michezo watakaza uzi inawezekana kabisa kufanyika matengenezo katika viwanja hivyo na Watanzania wakalifurahia soka.

Tunasema inawezekana kutokana na ukweli kwamba katika viwanja sita tulivyovitaja vyote ni nyasi bandia isipokuwa ule wa Taifa unaomilikiwa na serikali na CCM Kirumba wa chama tawala. Na karibu vyote vilivyosalia vinamilikiwa na CCM, ukiwamo Uwanja wa CCM Mkwakwani (Tanga), CCM Kambarage (Shinyanga) na Sokoine (Mbeya), mwingine ukiwa ule wa Sheikh Amri Abeid (Arusha) na Uwanja wa Namfua mkoani Singida. Kinachotushangaza ni kwa nini Kirumba unaomilikiwa na CCM kama vilivyo hivyo vingine umewezekana kuwa katika mazingira rafiki ya soka na vingine vishindikane?

Asilimia 15 ya mapato inayobaki kwa mmiliki wa uwanja katika kila mechi ni kwa viwanja vyote nchini, iweje CCM Kirumba iwezekane huku vingine ambavyo vinamilikiwa pia na CCM vishindikane kuboreshwa kuwa katika mazingira rafiki ya kuchezwa soka, ni kitu gani tunalazimishwa kukiamini hapa?

Tunatambua Rais John Magufuli, ambaye anatoka chama tawala kinachomiliki viwanja hivyo, ana majukumu mengi ya kufanya, hivyo wasaidizi wake wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, Waziri wa Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe wanapaswa kulitazama hilo, husussan asilimia hiyo 15 inapoelekezwa badala ya kuviboresha viwanja husika.

Lakini pia TFF inaonekana kulala sana katika mkakati wake wa kuhakikisha soka linachezwa katika viwanja vyenye sifa stahiki. Tunakumbuka wakati Singida United ilipopanda Ligi Kuu, ililazimika kuutumia Uwanja wa Jamhuri Dodoma kutokana na Namfua kutokuwa rafiki, na iliporejea Singida hali ilikuwa ya kuridhisha, lakini sasa umekuwa kama uwanja machungio ya ng'ombe na mbuzi.

Soka ni burudani na raha yake hukamilika linapochezwa katika uwanja rafiki wenye 'pitch' zinazoruhusu mpira kutembea, hivyo TFF, imefika wakati sasa kufungia viwanja vibovu hadi vitakapokarabatiwa, lakini pia wamiliki wa viwanja hivyo waelekeze mapato zaidi katika kuvikarabati na kama hilo limeshindikana ufike wakati sasa watafute wawekezaji ili viwe katika ubora stahiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

## BUSARA

**TUPONGEZE PANAPO PONGEZEKA**
KUMPONGEZA MTU NI KUMPA SIFA KWA KAZI NJEMA ALIYOIFANYA. KIMSINGI MTU HAPONGEZWI KWA KUTENDA MABAYA BALI HULAANIWA. HATA HIVYO TUSIWE WACHOYO WA KUPONGEZA PALE PANAPOSTAHILI KUPONGEZA. KUPONGEZA NI KUTOA MOTISHA NA MWELEKEO WA DIRA NJEMA. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tatizo Azam si makocha ni viongozi wenyewe

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara nyingine tena Azam FC imemtimua kocha mwenye heshima kubwa nchini Tanzania, Hans van der Pluijm, siku moja tu baada ya kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Simba kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pluijm, ametimuliwa akiwa hajamaliza hata msimu mmoja. Na cha ajabu ni kwamba pamoja na kutofanya vema kwa siku za karibuni, lakini rekodi bado zinaendelea kumbeba kocha huyo na kuonyesha kuwa hajafanya vibaya kiasi cha kutimuliwa.

Ndiye kocha aliyeiwezesha Azam kutwaa Kombe la Kagame mwaka jana, lakini mwaka huu akiwezesha kulichukua Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar kwa kuifunga Simba mabao 2-1.

Kwenye mechi za Ligi Kuu, Azam mpaka Pluijm anatimuliwa timu hiyo inakamata nafasi ya pili ikiwa na pointi 50 kwa michezo 25 iliyocheza, ikishinda mechi 14, sare nane na kufungwa mechi tatu.

Kwa hali ya kawaida haya bado ni mafanikio, lakini kwa viongozi wa Azam si mafanikio waliyoyataka.

Je, walitaka mpaka sasa Azam iwe inaongoza Ligi Kuu? Au wamemtimua kwa sababu tu wamefungwa na Simba? Au kutokana na kutofanya vema kwa michezo michache iliyopita?

Mkosi kwa Azam ulianza Februari 6, mwaka huu ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Alliance nyumbani Chamazi, mechi iliyofuata ikalazimishwa sare kama hiyo dhidi ya Lipuli, ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Prisons, ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Coastal, kabla ya kuchapwa mabao 3-1 na Simba.

Pamoja na kutofanya vema kwenye mechi hizi tano, lakini hiki si kigezo cha kocha huyo kutimuliwa kwa sababu hata Mtibwa haijafanya vizuri kwenye mechi kadhaa sasa kiasi cha kukamata nafasi ya 17, lakini bado viongozi wana imani na kocha wao, Zuberi Katwila.

Tatizo ninaloona ni kwamba viongozi wa Azam wanachukulia kuwa timu yao ni moja kati ya timu kubwa sawa au zaidi ya Simba na Yanga.

Ukweli ni kwamba kwa miundombinu Azam haifikiwi na timu yoyote nchini, lakini kwa uwanjani haitofautiani na Mwadui, Mtibwa Sugar au Biashara ya Mara.

Ina wachezaji wa kawaida sana na hata hao wa kigeni wanaoonekana wana uwezo mkubwa ni Yakubu Mohamed na Nicalaus Wadada tu.

Viongozi wa Azam badala ya kufukuza makocha kila kukicha, wajiangalie wao kwanza kwenye kioo, kwa kuwa hata aina yao ya usajili ni matatizo na makocha wengi wanaopewa timu huku wachezaji na si wao wanaowasajili.

Azam ina misimu 10 sasa kwenye Ligi Kuu ikiwa imeingia na kuwekeza moja kwa moja, lakini imetwaa ubingwa mara moja tu, huku ikiwa haijawahi hata kutinga Ligi ya Mabingwa.

Kwa timu kama yao sidhani kama inaweza kushindana na Simba ambayo msimu mmoja tu baada mwekezaji Mohammed "MO" Dewji kutangaza kuwekeza Sh. bilioni 20 na hata hivyo bado mfumo kuanza kazi rasmi, lakini tayari imetinga Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi.

Ilitegemewa mpaka sasa Azam iwe imefika mbali na yenye uwezo wa kununua mchezaji wa kiwango cha juu kwa thamani kubwa kuliko Simba, lakini imekuwa kinyume chake.

Badala ya kuwa kama TP Mazembe baada ya miaka kadhaa kama ilivyokuwa ikitabiriwa, imebaki ikipigania taji la Ligi Kuu bila mafanikio, na pia hata kiwango chao kimekuwa kikipungua na kutozitisha tena hata timu za mikoani kama ilivyokuwa zamani.

Makocha John Stewart Hall, Joseph Omog, Zeben Hernandez, Neider dos Santos, Itamar Amorin, Boris Bunjak na George Nsimbe, wote hawa waliondoka kwenye klabu hiyo kwa staili hii hii.

Sasa unajiuliza, tatizo ni makocha au viongozi wenyewe?

# BARUA/MJADALA

## Tuyalinde mazingira ya Tandale

**Mhariri habari**

*NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lilili na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.*

*Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisadia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.*

*Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.*

*Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi. Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Naziomba mamlaka za kiserikali zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.*

**Raia Mwema-Tandale**

## Walezi tusifuge tabia zisizokubalika

**Mhariri**

*KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao hawako tayari kusikiliza ushauri wa majirani juu ya tabia za watoto wao.*

*Katika mtaa ninaoishi Morogoro, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya wastaarabu.*

*Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu.*

*Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.*

*Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.*

*Kwamba wanaoenda kulalamika kwao wanamuonea gere kijana wao kutokana na maendeleo anayoyafanya.*


*Naomba serikali ya mtaa wetu ichukue hatua ya kumkanya kijana huyo ili aachane na tabia hiyo kwani inaweza ikamhatarishia maisha yake siku moja na hasa pale wananchi watakapojichukulia sheria mkononi.*

**Ramadhani Mloka- Morogoro**

### WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Simba ivaeni JS Saoura kama fainali




**Na Adam Fungamwango**

KIMAHESABU Simba bado ina nafasi nzuri ya kusonga mbele hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati huu ikiwa inakamata nafasi ya pili kwenye Kundi D kwa pointi sita.

Timu hiyo inazidiwa na vinara Al Ahly ambayo ina pointi saba. Machi 9, mwaka huu, Simba inakwenda ugenini kucheza dhidi ya JS Saoura ya Algeria kwenye mechi inayotarajiwa kuwa ngumu.

Tangu ilipofungwa mabao 3-0 dhidi ya Simba, Saoura haijafungwa mechi yoyote ili ikicheza nyumbani au ugenini.

Imejikusanyia jumla ya pointi tano na kushika nafasi ya tatu, huku AS Vita ikiwa na pointi nne.

Kwa mahesabu yalivyo, Simba hata ikifungwa nchini Algeria na kushinda mechi ya mwisho dhidi ya AS Vita inawezekana kabisa ikasonga mbele kwenye kundi hilo kwa kushika nafasi ya pili endapo Waalgeria hao watapoteza mechi yao ya mwisho ugenini dhidi ya Al Ahly ama kutoka sare.

Hata hivyo, viongozi wa Simba, benchi la ufundi na wachezaji wao wasijidanganye kutaka kusubiri mechi ya mwisho ili kujua hatma yao.

Simba ikitaka kufuzu hatua ya robo fainali bila presha, inatakiwa ijifunge kibwebwe na kwenda Algeria kucheza na Saoura huku ikiwa imekamilika kila kitu, kimbinu na kisaikolojia.

Viongozi wa Simba na wachezaji wao wanapaswa waache kila kitu na kuichukulia mechi hiyo kama fainali ya wao kusonga mbele.

Iwe inahitaji matokeo mawili tu kwenye mechi hiyo, kushinda au kutoka sare tu basi. Isiende 'kikondoo' kama ilivyokwenda kwenye mechi nyingine na kupoteza kirahisi tena kwa mabao mengi (5-0 ugenini dhidi ya AS Vita na kisha Al Ahly).

Simba inapocheza ugenini inaonekana kuwa ni tofauti kabisa na inapocheza nyumbani. Kwa nini? Kuna kitu kinakosewa. Na nani?

Ni viongozi wanaotangulia kwenye kuweka sawa mipango kama vile hoteli watakayofikia na maandalizi mengine? Ni mbinu za benchi la ufundi ambalo halina mfumo mzuri kwa wachezaji wao wanapocheza ugenini? Au wachezaji ambao huingiwa na woga wanapokuwa wanacheza ugenini?

Hapa jawabu inabidi litatuliwe kabla ya mechi hiyo ili Simba iende nchini Algeria ikiwa kamili kwa ajili ya kuivaa timu hiyo kutafuta ushindi au sare. Haitakiwi kwa namna yoyote ile kwa viongozi na wachezaji wa Simba kufikiria kuwa wasubiri mechi ya mwisho ndipo kuamua hatma yao.

Waifanye mechi dhidi ya JS Saoura kuwa kama fainali ya Kombe la Afrika linalochezwa ugenini.

Maandalizi ya mechi hiyo na uchezaji wake uwanjani uwe kama ni mechi ya mwisho ambayo kama isipopata matokeo mazuri, basi imetolewa kwenye michuano hiyo.

Ikumbukwe kuwa Simba mwaka jana ilitoka sare ya bila kufungana ugenini dhidi ya Al Masry ya Misri baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 nchini Tanzania kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, tena ikiwa na wachezaji wa kawaida sana, sembuse kwa sasa ambapo imeongeza baadhi ya wachezaji wa ndani na wa kigeni wenye uwezo mkubwa? Kwa mfano huo tu, basi inawezekana kabisa kwa Simba kwenda kupata matokeo mazuri ugenini kama kila mmoja kwenye nafasi yake atawajibika.

Ikipata matokeo mawili kati ya hayo, kushinda au sare, Simba itakwenda kucheza mechi yake ya mwisho dhidi ya AS Vita bila presha kubwa kwani mawili kati ya haya yanaweza kutokea.

Kama ikishinda inawezekana kabisa kukawa na uwezekano wa kukata tiketi moja kwa moja kabla ya mechi ya mwisho, lakini ushindi au sare unaweza kusababisha Simba ikahitaji sare tu kwenye mechi ya mwisho ili kufuzu.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Baba afurahia mwanawe kufungwa jela miaka 30

INATOKA UK. 3

hasa pale wanapofanyiwa vitendo hivyo na wazazi wao.

Alisema kitendo alichofanya mtoto wake dhidi ya mjukuu wake ni cha kikatili na kimeiletea aibu familia yake.

"Kwa kweli enzi zetu sisi yaani ile miaka ya zamani hakukuwa na mambo kama haya ya ajabu, mzazi kumbaka mwanawe wa kumzaa kisa kaambiwa na mganga ili apate utajiri," alisema na kuongeza:

"Mambo kama haya sisi ndio kwanza tunayaona siku hizi zamani hayakuwapo kabisa kwa hili mimi naipongeza serikali imetenda haki kabisa."

Mzee Katembo alisema siku ya kwanza alipopata taarifa ya kuwa mjukuu wake amebakwa na baba yake mzazi na binti huyo kulazwa katika hospitali ya Mision ya Ndanda mjini Masasi, alipoteza fahamu kwa vile katika maisha yake hakuwahi kusikia jambo kama hilo la baba kumbaka mtoto wake wa kumzaa.

Aliongeza kuwa hata alipokuwa akifunga safari ya kwenda hospitalini Ndanda kwa ajili ya kumuona mjukuu wake anaendeleaje baada ya kulazwa pia alipokuwa akiingia ndani ya hospitali hiyo, alikuwa akianguka na kupoteza fahamu kwa mara mbili mpaka tatu ndipo anapata fahamu.



Mkandarasi akitengeneza barabara inayounganisha Halmashauri ya Ushetu na Halmashauri ya Mji wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, ikiwamo Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora jana. PICHA: SHABAN NJIA

# Sirro: Mauaji ya watoto yatagharimu fedha nyingi

INATOKA UK. 3

alisema.

Bila kutaja kiasi cha fedha kitakachotumika, alisema kwa sasa kutakuwa na timu mbalimbali za uchunguzi ambazo zitaitaji fedha kutekeleza kazi hiyo.

Aidha, amewaonya waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi ambazo baadhi yake zimesababisha mauaji ya kikatili kwa sababu ya imani za kishirikina na kwamba wakibainika watashtakiwa kwa kesi za mauaji.

Operesheni hiyo ililenga kuangalia hali ya uhalifu hususani mauaji yanayotokana na imani za kishirikina.

Kwa kipindi cha miezi miwili jumla ya watoto 13 wameuawa katika mikoa ya Njombe na Simiyu, kwa kile kinachoelezwa ni imani za kishirikina na kulipiza kisasi.

# Vifo 25, ajali 7, miezi 9 magari ya serikali

INATOKA UK. 2

Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro.

Aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Salome Lukusi, Glory Mziray, Shaban Yusuph, Maria Buyenja, Msafiri Gerald, Hassan Kayuga, Sheila Shaban na ndugu wawili Silvester Mwakalebela na Rubaya Mwakalebela.

Aliwataka walionusurika katika ajali hiyo na kuwahishwa Hospitali ya St Francis Ifakara kwa matibabu, kuwa ni Faraja Gowele(30), Sauda Shaban(27), Stanislaus Budodi (27) na dereva wa gari hilo, Zefrini ambaye anashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Ihunyo alipongeza jitihada zilizofanywa na wananchi wa Kikwawila baada ya ajali kwa kuokoa majeruhi na kuopoa miili iliyokuwa imenasa kwenye gari hilo lililokuwa limezama mtoni.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya St Francis Ifakara, Dk. Antony Magoda, alikiri hospitali hiyo kupokea miili ya watu tisa juzi saa 12 jioni na majeruhi watatu ambao wote wamelazwa katika hospitali hiyo.

Dk. Magoda alisema hali za majeruhi hao zinaendelea vizuri baada ya kupimwa vipimo mbalimbali na kubaini hawana majeraha makubwa, na wako mbioni kuruhusiwa kuondoka hospitalini.

Majeruhi katika ajali hiyo, Sauda, Budodi na Gowele, kwa nyakati tofauti, walikiri chanzo cha ajali ni mwendokasi.

"Niliona gari likiwa katika 'speed' (mwendokasi) kali na tulipofika darajani, tushtukia gari inatumbukia mtoni, nilijitahidi kujinasua na kutoka," Sauda alisema.

**LUKUVI, LUGOLA WAOMBOLEZA**

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema amepokea kwa mshtuko na masikitiko taarifa ya ajali hiyo.

Alisema vifo vya watumishi hao waliokuwa wameajiriwa na mradi wa LTSP, ni pigo kubwa kwa taifa kwa vile limepoteza nguvu kazi ya taifa kutokana na wengi waliokufa kuwa ni vijana.

Alisema kwa niaba ya serikali na watumishi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, anatoa pole kwa wafiwa wote, wazazi, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wao na kuahidi serikali itahakikisha miili ya marehemu wote inasafirishwa na kuzikwa kwa mujibu wa taratibu.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, pia alitoa pole kwa Waziri Lukuvi, ndugu, jamaa na marafiki wa familia za watumishi hao.

"Natoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi, ndugu, jamaa na marafiki waliowapoteza wapendwa wao katika ajali hii. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina," Lukuvi alisema katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana.

**MIEZI 9 YA MAJONZI**

Ni ajali inayotokea katika kipindi ambacho Watanzania bado hawajasahau kuondokewa na maofisa watatu wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) waliofariki dunia baada ya gari lao kupata ajali eneo la Chalinze mkoani Pwani wakiwa njiani kwenda Dodoma miezi tisa iliyopita. Ajali hiyo ilitokea Mei 22, mwaka jana.

Vilevile, miezi miwili baadaye (Julai 30, mwaka jana), maofisa wawili wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, akiwamo ofisa habari wa wizara hiyo, Shadrack Sagati, walifariki baada ya gari lao kupinduka wilayani Chato mkoani Geita.

Wiki moja baada ya ajali hiyo ya Chato, Agosti 4, mwaka jana, gari la Wizara ya Maliasili na Utalii lilipata ajali mkoani Manyara na kusababisha kifo cha ofisa habari wa wizara hiyo, Hamza Temba. Katika ajali hiyo, Waziri wake, Dk. Hamis Kigwangalla alijeruhiwa.

Pia, Oktoba 20, mwaka jana, ikiwa ni miezi miwili baada ya ajali ya Manyara kutokea, watumishi watano wa Wizara ya Kilimo, walifariki dunia katika ajali ya gari baada ya kuacha njia na kupinduka Manyoni mkoani Singida.

Wiki mbili baadaye (Novemba 3, mwaka jana), watu watano ambao ni ndugu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), walifariki dunia katika ajali iliyohusisha magari mawili ya serikali, wakati wakitoka kumzika mama yao.

Ajali hiyo ilitokea katika Kijiji cha Mbwande wilayani Kongwa mkoani Dodoma, iliyohusisha gari la Ofisi ya CAG na la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ambalo abiria wake walijeruhiwa.

**Imeandikwa na Idda Mushi (MOROGORO) na Salome Kitomari (DAR ES SALAAM).**

# Majaliwa azungumzia utekelezaji ahadi za JPM

INATOKA UK. 3

maeneo yote nchini. Wananchi wote wanapata huduma sawa bila ya ubaguzi wa aina yoyote, hivyo endeleeni kuiamini serikali yenu."

Kadhalika, alisema wilaya hiyo imepewa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya na kuhusu upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa sasa umefikia asilimia 95.

Awali, Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Kibong'oto, Dk. Riziki Kisonga, alisema ujenzi wa jengo hilo utafanyika kwa awamu tatu, awamu ya kwanza itagharimu Sh. bilioni 2.183 na ilianza Septemba 2018 na inatarajiwa kukamilika Julai mwaka huu.

Alisema jengo hilo ni la ghorofa tatu zenye pande mbili pacha, upande wa kwanza ni kwa ajili ya kazi za maabara kwa uchunguzi wa vimelea hatari na hatarishi sana na virusi vinavyosababisha milipuko ya magonjwa kama marburg, ebola, chikungunya na dengue.

Alisema mradi huo mpaka kukamilika unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 8.86, ambazo zinaonekana kuwa zipo juu kutokana na uhitaji wa kitaalamu wa uwekaji wa mifumo thabiti ya kuchuja hewa ambayo itahimili kazi zinazotarajiwa kufanyika.

"Umuhimu wa maabara hii ni kusaidia kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ambukizi yakiwamo ya kifua kikuu na magonjwa mengine yasiyoambukiza katika ubora unaotambulika kimataifa."

Dk. Kisonga alisema maabara iliyopo hospitalini hapo kwa sasa imepata ithibati ya kimataifa ya kufanya vipimo vya ngazi ya daraja la pili, hivyo baada ya kukamilisha ujenzi huo watakuwa na uwezo wa kufanya vipimo vya ngazi ya daraja la tatu.

Alisema maabara hiyo itakapokamilika, watatoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mapya, ambayo ni hatarishi kwa usalama wa taifa na kimataifa hasa tatizo kubwa la usugu wa vimelea kwa dawa zinazotibu magonjwa mbalimbali.

## Mtanzania ang'ara misitu kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTANZANIA ambaye ni mtaalamu wa mazingira, Dk. Richard Stanslaus Muyungi, ameteuliwa kuwa mjumbe wa kamati huru ya kimataifa inayoshughulikia masuala ya utafiti wa misitu na miti (ISC).

Dk. Muyungi ambaye amefanya kazi kama mshauri mwandamizi wa masuala ya mazingira kwa miaka 25 sasa akijihusisha zaidi na masuala ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Mtaalamu huyo amesoma vyuo kadhaa nchini na nje kikiwamo Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Reggio Calabria nchini Italia na Chuo Kikuu cha Edinburgh. Amekuwa akijihusisha zaidi na utafiti juu wa sera za kimataifa za mazingira na utawala chini ya Umoja wa Mataifa (UN) haswa kupitia taasisi ya mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya mabadiliko ya tabianchi (UNFCCC), katika maeneo yanayohusiana na fedha zinazotolewa kwa ajili ya kushughulikia mabadiliko ya tabia nchi, kujenga uwezo na kupunguza madhara ya mabadiliko hayo.

Dk. Muyungi pia amefanya kazi UNFCCC kama mwenyekiti wa taasisi inayohusiana na masuala ya ushauri wa kisayansi na teknolojia ijulikanayo kama (SBSTA) kati ya mwaka 2011 na 2013 akiwa anashughulikia masuala yanayohusiana na mijadala ya kisayansi kusaidia utekelezaji wa upunguzaji wa madhara ya mabadiliko ya tabianchi duniani, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba taarifa za kisayansi zinatumika kwenye sera ngazi ya serikali mbalimbali. Pia ana uzoefu mkubwa kwenye gazi ya kitaifa na Bara la Afrika kwa ujumla. Hivi karibuni amekuwa akijihusisha na utafiti juu ya kutatua matatizo yanayoikumba sekta ya nishati nchini yanayotokana na changamoto za kimazingira ikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

# TPSF yatoa neno kwa serikali mazingira uwekezaji

**Na Beatrice Moses**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeipongeza serikali kwa kuonyesha nia madhubuti ya kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alisema kuna ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuimarika kwa majadiliano kati yao na serikali.

"TPSF imeshuhudia utayari na mwitikio mkubwa kwa upande wa serikali kukutana na kujadiliana na sekta binafsi katika ngazi zote za wilaya, mikoa na taifa na tayari mafanikio yameanza kuonekana," alisema Simbeye.

Aliongeza: "Mojawapo ya mafanikio ambayo TPSF inajivunia ni kuimarika kwa majadiliano yenye tija kati ya sekta ya umma na sekta binafsi," alisema Simbeye.

Alisema mawaziri kama wanane wanaendelea kupita mikoa mbalimbali, ambapo pamoja na mambo mengine wanatumia muda huo kuzungumza na wadau wa sekta binafsi.

Simbeye amewataka wadau hao kujitokeza kwa wingi wanapoitwa na mawaziri hao, ili watumie nafasi hiyo kuwatoa mawazo yao yatakayosaidia kuzidi kuboresha mazingira ya biashara.

Alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wafanyabiashara kutochanganya siasa na biashara, akibainisha kuwa taasisi hiyo ikibaini itawafuta uanachama.

Alisema pia TPSF imekusudia kujadili mambo mbalimbali na wadau wake, ikiwamo jinsi wanavyoweza kupandisha kiwango kinachochangia sekta binafsi kwenye pato la taifa kutoka asilimia 12 hadi asilimia 15 au zaidi.

Simbeye alisema wameandaa mikutano kwa ngazi ya kanda kuanzia Machi hadi Mei mwaka huu, utakapofanyika mkutano wa kitaifa, ambapo wataitumia kujadili mambo hayo pamoja na kujitathmini jinsi wanavyotoa ajira na kuchangia pato la taifa kwa ujumla.

Alisema kama wadau wakuu wa maendeleo nchini wanapaswa kuhakikisha wanainua pato la taifa ikiwezekana hata kuifikia Kenya, ambapo sekta binafsi inachangia pato hilo kwa asilimia 18.

Alitoa mfano wa uwapo mkutano kama ule uliofanyika hivi karibuni wa asasi ya wachimbaji wa madini wadogo (FEMATA), waliwasilisha changamoto zao kwa mheshimiwa Rais na kupatia ufumbuzi kama vile kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya zuio.

Alisema kutokana na hatua hiyo nzuri TPSF ilipanga kufanya majadiliano ya kitaifa yanayojumuisha wadau wa sekta binafsi mwishoni mwa Februari.

"Mwitikio umekuwa mkubwa, wamejitokeza wadau 250 wa sekta binafsi wakati tulikuwa tumejipanga kutumia ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, ambao uwezo wake ni kuchukua watu 1,000, hivyo hapatoshi," alisema Simbeye.

Alisema kutokana na hali hiyo wameamua kuanza na mkutano ngazi ya kanda kuanzia Machi, watajadili mambo mengi ikiwamo Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga, Kanda ya Mashariki ambayo mikoa ni Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Simbeye alitaja kanda nyingine kuwa ni Kanda ya Kati ambayo ni Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Rukwa na Katavi na Kanda ya Kusini ikiwa ni Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Alisema pia Kanda ya Ziwa iliyo na Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza na Simiyu, pia itajumuisha Visiwani Zanzibar na kumalizia na mjadala wa kitaifa unaotarajiwa kufanyika Mei mwaka huu.



Meneja wa Chama kikuu cha Ushirika Igembesabo mkoani Tabora, Emmanuel Malunde, akichangia mada kwenye kikao cha wadau wa zao la pamba mjini Shinyanga, ambacho kilikutanisha mikoa sita kujadili namna ya kuimarisha vyama vya ushirika na kuboresha zao hilo na kulalamikia kuwapo na ubadhirifu wa fedha kwenye vyama vya msingi vya ushirika mkoani Tabora. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aonya watumishi kujiepusha rushwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imewataka watumishi wa umma kutojihusisha kushiriki vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria pamoja na kupoteza ajira.

Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), George Mkwichika, wakati akizungumza na watumishi mbalimbali wa umma kwa wilaya za Liwale na Nachingwea mkoani Lindi. Waziri Mkwichika alisema hayo alipokuwa katika ziara kuzungumza na watumishi wa umma na kuangalia utekelezaji wa miradi unaofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia nguvu kazi ya wananchi. Alisema ni vema kila mtumishi akajiepusha na rushwa badala yake waendelee kuhudumia jamii ili kuondoa manung'uniko.

Alisema watumishi wamekuwa wakionywa dhidi ya vitendo vya rushwa kuanzia serikali ya awamu ya kwanza kwa kueleza kwamba rushwa ni adui wa haki, ndio maana imeundiwa chombo maalum kinachoshughulikia vitendo hivyo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Waziri Mkuchika alisema kwa mujibu sheria, mtoaji na mpokeaji rushwa wote wana makosa, hivyo wanapokamatwa wanafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayowakabili. "Kama hakuna mtoaji au mpokeaji, rushwa haina nafasi ya kusambaza mizizi yake," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuchika, serikali ya Rais John Magufuli imekuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya watumishi wa umma wanaoendeleza hali hiyo kwa lengo la kuirejeshea nchi kwenye heshima yake.

HABARI KITAIFA

# AMCOS vyadaiwa kutafuna mil. 122/-

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VYAMA vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) mkoani Tabora, vimedaiwa kutafuna kiasi cha shilingi milioni 122 za ushuru wa zao la pamba, katika msimu wa kilimo uliopita wa mwaka (2018-19) na kukitia hasara chama kikuu cha ushirika mkoani humo.

Imeelezwa vyama vya msingi mkoani Tabora vipo 118, lakini vilivyolipa ushuru wa zao hilo la pamba kwenye chama kikuu cha ushirika mkoani humo ni 16 na vimelipa nusu, huku vingine vikitafuna fedha zote na kufanya kuwapo na ubadhirifu wa shilingi milioni 122.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na meneja wa chama kikuu cha ushirika Igembesabo mkoani Tabora, Emmanuel Malunde, kwenye kikao cha wadau wa pamba Kanda ya Ziwa kilichokutanisha mikoa sita ya Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Tabora na Mara.

Alisema katika msimu wa kilimo wa zao 2018-19) kumekuwapo na tatizo kwa baadhi ya vyama vya msingi vya ushirika mkoani Tabora, kutafuna fedha zote za ushuru wa zao hilo na kutolipa hata kidogo, huku viongozi wao wakikimbilia kusikojulikana.

"Mwenyekiti, serikali imekuwa ikijitahidi sana kufufua vyama hivi vya msingi vya ushirika ili mkulima apate kuuza mazao yake kihalali na kuinuka kiuchumi, lakini kuna baadhi ya viongozi wa sio waaminifu kabisa, hawapo kwa ajili ya kumkomboa mkulima, bali ni kujinufaisha wenyewe kwa kufanya ubadhirifu wa fedha," alisema Malunde. "Mfano mkoani Tabora kuna vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) 118, lakini vilivyolipa fedha za ushuru wa zao la pamba ni 16 shilingi milioni 70.5, na vilivyosalia vyote havijalipa, huku vingine viongozi wake wakikimbia sababu wameshakula fedha zote, ambapo kwa sasa tupo kwenye msako wa kuwakamata," aliongeza.

Mwenyekiti wa kikao hicho Kaimu Mrajisi kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Wizara ya Kilimo, Charles Malunde, alitoa maagizo kuwa chama chochote cha msingi cha ushirika ambacho kimefanya ubadhirifu wa fedha, hakuna kununua pamba katika msimu ujao pamoja na kuwachukulia hatua viongozi.

Alisema suala la upigaji madili kwenye vyama vya ushirika lilishapitwa na wakati, na kiongozi ambaye ataingia kwenye vyama hivyo ajitathmini kwanza, ambapo kwa sasa serikali inahitaji kuleta mabadiliko kwenye ushirika ikiwa ndiyo mkombozi mkubwa wa mkulima katika kumuinua kichumi na taifa kwa ujumla.



Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani na Kilimo Mkoa wa Tanga 'TPAWU', Mrefu Adriano, akizungumza na wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza magunia yatokanayo na nyuzi za mkonge Tancord, kilichoko eneo la Ngomeni Muheza, nje ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, wafanyakazi hao waliandamana jana wakidai mishahara ya miezi mitatu. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

# TGNP Mtandao kupinga ukatili dhidi ya watoto

**Na Yasmine Protace**

KUTOKANA na kuongezeka kwa matukio ya ukatili kwa watoto, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), inatarajia kuzindua kampeni ya kupinga ukatili kwa watoto kwa kuanza kuzunguka katika maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalisemwa na Anna Sanga, ofisa mpango wa harakati na ujenzi wa nguvu za pamoja kutoka TGNP Mtandao.

Sanga alisema kuwa, watoto wamekuwa wakifanyiwa ukatili na kwamba matukio hayo yamekuwa yakitokea kila uchao.

"Kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili utaanzishwa umoja wa watu usiopungua 100 ambao watakuwa na beji, na umoja huo utatumika kupinga ukatili," alisema.

Aliongeza kuwa, wataanzisha kampeni ya juu ya kupinga ukatili kwa watoto.

Alisema, ukatili kwa watoto umekuwa ukiongezeka siku hadi siku, hivyo ili kufanikisha kuondoa vitendo vya ukatili kwa watoto, kampeni hiyo itatumia kutoa elimu, na kwamba watazunguka maeneo mbalimbali ya nchi kwa kuwahamasisha wananchi kuachana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

# Kamata mkaa yaathiri mapato ya halmashauri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamesema kushuka kwa makisio ya mapato ya Idara ya Maliasili unatokana na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuwakamata wauzaji wa mkaa ambao wamekuwa wakipeleka mikaa wilayani Kahama wakitokea katika halmashauri hiyo.

Madiwani hao waliyabainisha hayo juzi, kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya pili ya halmashauri hiyo, ambapo walisema kuwa mwaka wa fedha 2018/19 idara hiyo ilikusanya fedha zaidi ya asilimia 105 na kupelekea kuweka mikakati ya kuwanunua gari.

Sharifu Samul, Diwani wa Kata ya Kinamapula, alisema kuwa, kushuka kwa mapato ya idara hiyo kutoka asilimia 105 kwa mwaka wa fedha ulipitia hadi kufikia asilimia 25 kwa robo ya pili sawa na shilingi milioni 64.749 kunatokana na wakala wa huduma za misitu kuendelea kuwakamata wauzaji wa mkaa.

Alisema kuwa, kama TFS itaendelea kuwakamata wauzaji wa mkaa na kuwachukulia hatua ikiwamo kuwanyang'anya mkaa wao, idara hiyo itashindwa kutimiza malengo ya makusanyo ya shilingi milioni 257.5 ambazo zinatarajia kukusanywa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019 hadi 2020.

"Mwenyekiti, idara ya maliasili ni idara nyeti sana ambayo inategemewa na halmashauri katika vyanzo vyake vya mapato ukiachilia idara ya kilimo pamoja na idara ya biashara, tunaomba mkurugenzi kukutana na watu wa TFS kuangalia namna ya kulitatua jambo hili," alisema Samuel.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Nyankende, Doa Limbu, alisema kuwa, mbali na kuwakamata na kuwachukulia hatua ongezeko la ushuru umekuwa mkubwa ambapo halmashauri huwatoza kiasi cha shilingi 1,000, huku wakala wa huduma za misitu wakiwatoza kiasi cha shilingi 12,000 kwa kila gunia.

Pia Limbu alisema, kwa sasa wauzaji wa mkaa wamekuwa wakikwepa kulipa ushuru na kutumia njia za panya kupeleka mkaa wao sokoni na kuongeza ugumu, kama jambo hili lisipotatuliwa idara ya maliasili itazidi kupoteza mapato na kulaumiwa na madiwani kuwa hatufanyi kazi.

Akijibu hoja hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Michael Matomora, alikiri wakala huo kuwakamata wauzaji wa mkaa na kudai jambo hilo ameshalifikisha kwa mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ili kuangalia namna ya kulitafutia ufumbuzi.

# Teknolojia kugundua aina ya magonjwa ya mazao dakika 20

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAKULIMA wametakiwa kutoa taarifa haraka kwa wataalamu wa kilimo wanapogundua mazao yao yanashambuliwa na magonjwa au wadudu, ili waweze kupatiwa majibu kwa muda wa dakika 20 hadi 48 kwa kutumia teknolojia mpya ya vinasaba (DNA).

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania kutoka kituo cha Selian Dk. Joseph Ndunguru, wakati wakitoa mafunzo kwa wataalamu watafiti wa kilimo na wanasayansi toka Kituo cha Utafiti Selian (SARI), watafiti Chuo cha Tengeru na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, jinsi ya kutumia teknolojia ya DNA katika kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao.

Alisema teknolojia hiyo ina uwezo wa kugundua aina ya ugonjwa na wadudu waliopo na kutoa majibu ndani ya dakika 20 hadi saa 48 kutegemea na ukubwa wa tatizo.

"Teknolojia hii iliyozinduliwa mwaka jana Butiama ina mwakikishia mkulima kufahamu tatizo mara moja na kulipatia ufumbuzi, jambo litakalowezesha wakulima kupata mazao yenye tija tofati na zamani ilichukua muda mrefu kupata majibu," alisema.

Aidha, alisema zamani walikuwa wakichukua muda mrefu kugundua tatizo kutokana na kulazimika kuchukua sampuli shambani wapeleke maabara na kupata majibu baada ya kuchukua muda mrefu.

Alisema lakini usumbufu huo umeisha mwaka jana baada ya serikali nchini kupitia vituo vya utafiti Mikocheni kwa kushirikiana na wataalamu wa nchini Australia kuja na teknolojia ya DNA.

Dk. Nduguru alisema teknolojia hiyo licha ya kugundua wadudu na magonjwa wanaoshambulia mazao, pia inauwezo kubaini magonjwa ya binadamu, samaki, wanyamapori na kutambua aina mbalimbali za mimea ya porini.

Alitoa wito kwa wataalamu wa kilimo na mifugo wa kila wilaya kuwa na kifaa hicho cha DNA kwa ajili ya kupimia, kwa sababu gharama yake ni dola za Marekani 1000 kwa kifaa kimoja chenye uwezo wa kupima wilaya nzima.

Kwa upande wake, mwezeshaji wa mafunzo hayo ambaye ni mtafiti wa kilimo kutoka kituo cha Mikocheni cha Dar es Salaam, Charles Kayuki, alisema kupitia kipimo hicho wataweza kubaini aina ya virusi na wadudu wanaosumbua na kutoa majibu kwa mkulima ndani ya dakika 20 hadi 48 tofauti na zamani walikuwa wakitoa majibu zaidi ya miezi sita.

Benjamini Steven wa Kituo cha Utafiti cha Tengeru (TARI), alisema mkulima atarajie kupata mazao mengi kwa sasa sababu hakuna kitakachomsumbua bila kupata majibu ndani ya muda mfupi kabla mazao hayajaharibika.

"Na tunachotaka kufanya kwenda kila mkoa na kanda kutafiti aina za magonjwa yanayosumbua wakulima na kuwashauri wakulima kwa mkoa au kanda husika aina ya mimea ya kulima kulingana na magonjwa yalioko.

# Mawaziri wakusanya maoni ufumbuzi mgogoro wa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

MAWAZIRI saba wametembelea Kijiji cha Kimotorok wilayani Simanjiro, kukusanya maoni na mapendekezo ya kutatua mgogoro wa muda mrefu wa mpaka wa ardhi baina ya wananchi wa eneo hilo, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero.

Aidha, mawaziri hao wamesikiliza mgogoro wa ardhi wa Kijiji cha Irkushbor cha wilayani Kiteto na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero.

Mwenyekiti wa mawaziri hao, William Lukuvi ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema mwishoni mwa wiki kuwa walitumwa na Rais John Magufuli kusikiliza mgogoro huo.

Alisema baada ya kupokea mapendekezo ya namna ya kumaliza mgogoro huo kutoka pande zote watafikisha suala hilo kwa Rais Magufuli ili atoe maamuzi.

Alisema wamepokea maoni kutoka kwa wananchi wa vijiji hivyo, viongozi wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya, wabunge, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero.

"Baada ya kupokea mapendekezo haya kwa njia ya maandishi na maoni ya mdomo tumeandika na tutayapeleka kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri na kisha aliyetutuma atayatolea maamuzi," alisema. Pamoja na Lukuvi, wengine aliongozana nao ni Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima. Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamisi Kigwangala, hakuhudhuria kutoka na kifo cha mwanaye.

Mwaka jana Waziri Kigwangalah aliagiza wananchi wa Kijiji cha Kimotorok wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero kuondoka eneo hilo ifikapo Septemba, lakini Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akawaambia wananchi hao wasiondoke.

Akizungumza mbele ya mawaziri hao, Mnyeti alisema amekagua nyaraka zote zilizoko kwenye mkoa huo, lakini hajakuta sehemu inatamkwa kuwa Pori la Akiba la Mkungunero liko Manyara.

Alisema baadhi ya wafugaji wa Kijiji cha Kimotorok wilayani Simanjiro na Irkushbor wilayani Kiteto, wanafukuzwa mara kwa mara na wamenyang'anywa mifugo yao zaidi ya 600.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James ole Millya, alisema wananchi hao wamenyanyasika vya kutosha kwa kuwa kila wakati wanafukuzwa na kuambiwa wapo hifadhini.

Alisema ni wakati sahihi wa kuweka mpaka ili ijulikane mwisho wa wafugaji hao na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero, kuliko mpaka wao kusogezwa kila wakati.

"Kwa sababu mmekuja na helikopta mnaweza kupita juu na kuona mifugo yetu ng'ombe na mbuzi zinachungwa pamoja na wanyamapori wakiwamo tembo, pundamilia, swala na nyumbu sisi wamasai ni wahifadhi wazuri," alisema.



Mkazi wa Dar es Salaam akiwa anatembeza viatu barabarani kutafuta wateja ikiwa ni jitihada ya kujikwamua na umaskini. Awali biashara hiyo ilikuwa inafanywa na vijana wa kiume. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Diwani Chadema aungana na wadau

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

TATIZO la kutengeneza na kunywa pombe haramu maarufu gongo au pure lililokuwa limeikabili Kata ya Ngarenaro jijini hapa, limeanza kuvaliwa njuga baada ya wananchi kupatiwa elimu ya kuacha kuitengeneza na kupewa ubunifu wa kufanya biashara zingine.

Unywaji wa kukithiri wa pombe hiyo umechangia kuzorota kwa shughuli za maendeleo kutokana na wanywaji wengi kutokuwa na afya ya kufanya kazi.

Akizungumza ofisini kwake juzi, Diwani wa Kata ya Ngarenaro, Isaya Doita, (Chadema), alisema kwa muda mrefu kata hiyo ilikuwa ikisifika kwa upikaji na unywaji wa gongo.

Alisema sasa hivi changamoto hiyo imemalizika kutokana na kutolewa kwa elimu mbalimbali.

Alisema kutokana na changamoto hiyo amekuwa akitoa elimu akishirikiana na wadau mbalimbali kwa wananchi wa kata hiyo ambao wameweza kuacha vitendo hivyo na kujiunga na biashara zingine za kuwapatia kipato kwa kuwa wengi wao walikuwa wakitegemea gongo hiyo kujipatia kipato.

"Kwa kweli Ngarenaro ya sasa hivi siyo ile ya zamani ya watu kulewa gongo kuanzia asubuhi hadi jioni, sasa hivi watu wanafanya shughuli za maendeleo baada ya kupatiwa elimu kutoka kwa wadau mbalimbali na kuachana na upikaji huo wa gongo," alisema. Aidha, alisema pombe hiyo ilikuwa ikichangia kuporomoka kwa elimu katika kata hiyo kutokana na wanafunzi wengi kunywa pombe kupita kiasi na kuweka kwenye chupa za maji bila watu kujua.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baadhi ya wananchi wa kata hiyo, Laurence Kivuyo, alisema kata hiyo ilikuwa maarufu kwa upikaji na unywaji wa gongo, ambapo sasa hivi limedhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Alisema kumekuwapo na wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakitoa elimu ya madhara ya unywaji na upikaji wa gongo, ambapo wengi wao wameweza kubadilisha mtazamo na kujishughulisha na biashara zingine za kuweza kuwapatia kipato.

Naye Upendo Mollel alisema baada ya kutolewa kwa elimu hiyo wameweza kuleta mabadiliko makubwa ya watu kuwa na shughuli halali za maendeleo.





# Jukwaa lahimiza kuanza vituo huduma za pamoja

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUKWAA la majadiliano ya kisera la Mkoa wa Kilimanjaro, limetaka watendaji wakuu wa serikali katika halmashauri saba za mkoa huo wasicheleweshe agizo la uanzishwaji wa vituo vya huduma za pamoja katika hospitali za wilaya ifikapo Machi 31, mwaka huu, ili kutoa fursa ya kuhudumiwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Azimio hilo pamoja na hoja ya kutaka kutengwa kwa ruzuku ya kuziwezesha kamati za utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ni miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na kuazimiwa na jukwaa hilo kwa mwaka 2019.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tusonge linaloratibu jukwaa hilo, Agnatha Rutazaa, alisema azimio la kutaka kuanzishwa kwa 'one stop centre' limetolewa na wadau hao baada ya kukaa pamoja na watoa maamuzi katika ngazi za halmashauri, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama na Jeshi la Polisi, Magereza na serikali ngazi ya halmashauri na mkoa.

"Lengo kuu la jukwaa hili ni kujenga jamii yenye usawa na usalama, ambapo watoto, vijana, wanawake na wadau wanashiriki kukuza, kulinda na kuheshimu haki za binadamu. Katika hili tunalenga zaidi pia kuwasilisha mapendekezo kwa watoa maamuzi na wadau yanayolenga kukuza na kuendeleza Mtakuwawa (Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto)," alisema Rutazaa.


"Hawa wahanga wa ukatili wa kijinsia wamekuwa wanahangaika sana, mara wanatakiwa waanzie polisi wapate PF3 (fomu namba tatu), atoke pale aende akapate ushauri nasaha, atoke pale sasa aende akapate matibabu. Huo mzunguko ni mrefu sana, tumesema angalau kila wilaya iwe na one stop centre kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu."

Jukwaa hilo limeishauri serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2016 na utafikia ukomo mwaka 2022.

Pia, wadau hao kwa umoja wao wamekubaliana maombi ya ruzuku kwa ajili ya kutekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, yaanzie ngazi ya kijiji, mtaa, kata hadi ngazi ya halmashauri na mkoa. Katika hatua hiyo, wameafikiana kumhusisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupokea mapendekezo yatakayowasilishwa na ngazi ya mkoa.

Ofisa wa Dawati la Jinsia, Wanawake na Watoto wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Emmanuel Yohana, alisema Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya wanapaswa kuhakikisha vituo hivyo vya huduma za pamoja vinaanzishwa kama ilivyoelekezwa katika barua ya Mganga Mkuu wa Mkoa huo (RMO) Dk. Best Magoma, ya Januari 29 mwaka huu.

Kuhusu ruzuku inayopaswa kutengwa na serikali, ofisa kutoka Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) kwa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephano Msuya, alisema mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto unapaswa kuwa ajenda endelevu katika kila kikao na hivyo serikali haina budi kutenga fedha za kutekeleza mpango huo.



Mkurugenzi wa Kampuni za Kiluwa Group, Mohamed Kiluwa na Mwakilishi wa Kampuni ya Africa Jambo Group ya nchini Afrika Kusini, Marthinus Christiaan LandMan, wakibadilishana nyaraka za makubaliano ya ujenzi wa kiwanda chenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 150 cha kutengeneza mabehewa ya treni ya zamani na ya kisasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bosi TRA afunguka uzalishaji pombe kali

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Charles Kichere, amesema mwitikio mkubwa wa wazalishaji wa pombe kali kutumia mfumo wa kielektroniki kukidhi mahitaji ya lazima ya soko, ndio mwarobaini wa kuwadhibiti watengenezaji wa pombe zisizo na ubora. Idadi kubwa ya vinywaji hivyo vinazalishwa na viwanda bubu ambavyo havifikii ubora katika uzalishaji na hivyo kusababisha madhara kwa watumiaji, licha ya kuathiri soko la viwanda halali ambavyo vimethibitishwa na mamlaka za serikali.

Alikuwa akizungumza jana mjini hapa baada ya kufanya ukaguzi wa uzalishaji wa vinywaji na ufungaji wa mfumo wa kielektroniki katika kiwanda cha kutengeneza bia cha Serengeti na kiwanda cha pombe kali cha Banana na Highlife vilivyoko katika mji wa Moshi.

"Huu mfumo utawadhibiti kila kona watengenezaji wa pombe bandia ambazo hazina ubora kwa watumiaji na zinazoathiri soko la vinywaji vinavyotengenezwa na viwanda vilivyosajiliwa. Hili ndio suluhisho la tatizo lililoko sasa na tunatarajia mfumo huu utamaliza malalamiko ya wenye viwanda rasmi," alisema Kichere.

Wakati wa ukaguzi huo, menejimenti za viwanda hivyo kwa nyakati tofauti zimeeleza kwamba wana matumaini makubwa na mfumo huo na kwamba changamoto kubwa inayojitokeza sasa ni wazalishaji wa pombe za kienyeji ambazo zinaonekana kuathiri soko la vinywaji vya viwandani.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha High Life, Wilfred Tarimo, alisema iwapo mahitaji ya bidhaa hizo yatapungua sokoni kutokana na mfumo kushindwa kuvibana viwanda feki, kampuni zinazomiliki viwanda vya vinywaji zitalazimika kupunguza uzalishaji.

Kwa upande wake, Meneja wa Kiwanda cha Bia cha Serengeti, Geofrey Werema, alimweleza Kichere, kwamba viwanda vya bia na vinywaji vikali vinapambana na ushindani mkali kutoka kwa viwanda bubu vinavyozalisha pombe kinyume cha sheria, jambo linaloweza kuufanya uchumi ukashuka iwapo hali hiyo haitadhibitiwa.

# Majaliwa aagiza udhibiti magendo

**Na Mary Mosha,** ROMBO

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza vyombo vya usalama mkoani Kilimanjaro kuongeza kasi ya udhibiti wa bidhaa za magendo na wahamaji kutoka nchi za Afrika za wanaovuka kinyemela kupitia mpaka wa Holili.

Majaliwa alitoa agizo hilo juzi, alipokwenda kukagua kituo cha mpaka wa forodha cha Holili kilichoko Wilaya ya Rombo.

"Nimekuja kujua changamoto zenu, lakini kutoa maelekezo ya serikali ya nini kifanyike kuhakikisha taifa linaendelea kuwa salama. Ninazo taarifa kwamba mpaka huu huingiza baadhi ya bidhaa na watu ambao huingia kwa njia tofauti zikiwamo halali na zisizo halali," alisema.

Ametaka majeshi kwa nchi za Tanzania na Kenya kushirikiana na Idara ya Uhamiaji kujiridhisha kuhusu utendaji wao na kuanzisha mfumo wa pamoja wa kiusalama, ili kuhakikisha hakuna mtu anayeingia Kenya ama Tanzania na kufanya uhalifu wa aina yoyote.

Alitaka kitengo kinachohusika na ukaguzi na mizigo na vifurushi katika mpaka wa Holili kuwa waadilifu na wenye kutumia teknolojia kubaini bidhaa na silaha ambazo zingeweza kupitishwa kwa ujanja ujanja katika mpaka huo na kwenda kuleta athari Tanzania au Kenya.

Aidha, Waziri Mkuu aliwataka wananchi kufuata sheria pale wanapotaka kwenda upande mwingine wa nchi kwa kuwa kinyume na hapo watajiingiza matatani na hakutakuwa na msamaha.

Kwa upande wake, Meneja Usimamizi wa Forodha (Customs & Border Control) (CBC), Daniel Nyambaka, kutoka Kenya, alimwakikishia Waziri Mkuu kwamba udhibiti wa bidhaa ni mkubwa.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 25, 2019



USIYOYAJUA SIMBA VS AZAM FC TAIFA UK.15

## SAMBARATISHA...




### ISIKUPITE

KADI nyekundu ya Sergio Ramos aliyopewa Jumapili ya Novemba 17, mwaka huu wakati wakikubali kichapo cha mabao 2-1 kwenye La Liga nyumbani dhidi ya Girona ni ya 20 kwake katika michuano hiyo, na inamfanya kuwa mchezaji anayeongoza kwa kadi nyekundu katika historia ya michuano hiyo.

Lionel Messi (kushoto), akishangilia sambamba na Gerard Pique baada ya kukamilisha hat-trick yake wakati Barcelona ikiisambaratisha Sevilla kwao kwa kuichapa mabao 4-2 kwenye mechi ya La Liga juzi. **HABARI UK. 15**

# WAKALI WASIOKUBALIKA EPL



Lindelof

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England (EPL), ni moja ya ligi inayojulikana zaidi na kufuatiliwa zaidi duniani. Sababu kubwa ya umaarufu wake ni kwamba ina wachezaji wenye majina makubwa akiwamo Paul Pogba, Eden Hazard, Harry Kane. Lakini kila mchezaji mkubwa anakuwa na ndoto zake na kuwa mkubwa zaidi, ingawa wengine wanajikuta wakidharaulika.

Mfano mzuri zaidi ni Sergio Busquets pale Barcelona kwa muongo mmoja uliopita. Ingawa katika kipindi chake cha uchezaji amecheza na wachezaji wakubwa kama vile Lionel Messi, Andres Iniesta, Luis Suarez, Neymar, lakini bila yeye, Barcelona inaonekana ni kama isiyokamilika. Uwezo wake wa kucheza na mpira kwa akili ndio umekuwa chachu ya Barcelona kushinda mataji kadhaa kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao hawapewi nafasi kubwa zaidi licha ya viwango vyao kuwa muhimu zaidi kwa timu...

**1. Victor Lindelof**

Beki huyu wa kimataifa wa Sweden alijiunga na Manchester United kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2017 akitokea Benfica, lakini mara chache mno amepata nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza hasa kutokana na uwapo wa mkongwe Chris Smalling na Eric Bailly. Ameanza katika mechi 17 za Ligi Kuu msimu uliopita, lakini tangu kuondoka kwa Jose Mourinho, kocha wa sasa wa United, Ole Gunnar Solskjaer ameonyesha imani kubwa kwake. Tayari ameanza kwenye mechi 19 za Ligi Kuu msimu huu na ameonekana kuwa imara zaidi kwenye safu ya ulinzi.

Ameonekana kuwa mtu muhimu na msaidizi mzuri wa Luke Shaw wakati anapopanda kwenye winga ya kushoto. Hapewi sifa zake kutokana na sababu kwamba mabeki wa kati ndio wanaonekana kuwa na mchango mkubwa. Amekuwa mmoja wa wachezaji anayeokoa hatari nyingi zaidi kwa asilimia 4.3 kwa mchezo akiwa wa pili nyuma ya Chris Smalling.

**2. Aymeric Laporte**

Katika kikosi cha Manchester City chenye wachezaji wakali kama Kevin de Bruyne, David Silva na Sergio Aguero, kiwango cha Laporte hakiwezi kuonekana. Kwa sasa pengine ndiye mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi cha Manchester City baada ya Fernandinho. Manchester City wanacheza kwa kuwa na safu imara ya ulinzi, huku pia kocha, Pep Guardiola akisisitiza kusukuma mpira mbele. Na hilo linafanya timu iwezi kushaumbulia na mashambulizi ya kushitukiza na kama sio Laporte Man City ingekuwa kwenye wakati mgumu zaidi.

Lakini uwezo wake mkubwa zaidi ni usahihi wa pasi zake. Anacheza angalau pasi 86 za uhakika kwenye mchezo na kuwa wa pili nyuma ya Jorginho. Usahihi wa pasi zake ni asilimia 92.2 % na kumfanya kuwa mchezaji wa tatu kwenye ligi.

**3. Cesar Azpilicueta**

Katika misimu yake saba pale Chelsea, Azpilicueta amekuwa mmoja wa wachezaji anayeheshimika zaidi kwenye timu, lakini wengi hawampi umuhimu mkubwa hapo Stamford Bridge na si mbinafsi hasa anapokuwa dimbani. Kipindi chote cha uchezaji, Cesar amekuwa mtu muhimu zaidi katika safu ya nyuma ya Chelsea. Jose Mourinho alikuwa na imani kubwa kwake na kuna wakati aliwahi kusema: "Timu yenye wachezaji 11 kama Azpilicueta inaweza kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Cesar chini ya Antonio Conte, alionyesha ubora wake wa kucheza kwenye safu ya beki wa kati na bado hadi sasa ni mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho.

**4. Georginio Wijnaldum**

Mholanzi huyu alijiunga na Liverpool kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 akitokea Newcastle United pamoja na James Milner, na amekuwa nguzo kubwa kwa Liverpool kwenye safu ya kiungo. Wakati wa msimu wa 2016-17, alijiimarisha mwenyewe kama kiungo bora zaidi akifunga mabao sita kwenye ligi. Msimu uliofuata, Klopp alimfanya kuwa kiungo mkabaji baada ya Milner kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

Ingawa amefunga bao moja pekee, msimu huu pengine ndio bora zaidi kwake katika maisha yake ya uchezaji na mashabiki wa Liverpool wamekuwa na imani kubwa naye. Uwezo wa kumiliki mpira kwenye safu ya kiungo ni kubwa mno akiwa na asilimia 91.9% na ndio kubwa mno kwa kikosi cha Liverpool.

**5. Jan Vertonghen**

Tofauti na wachezaji wengine kwenye orodha hii, Vertonghen hajawa mchezaji mwenye kiwango kilekile, lakini kwa umri wake kuonekana kupevuka amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa kocha Pochettino. Pochettino anapenda kuwachezesha wachezaji kwa mzunguko na tangu amekuwa kocha wa Tottenham, Vertonghen ameimarika zaidi kiuchezaji. Wakati wa siku zake za mwanzo hapo Tottenham, alicheza kama beki wa kati ambaye amebakia katika nafasi hiyo kwa muda mrefu.

Chini ya Pochettino, uwezo wake uwanjani umezidi kuimarika na sasa amekuwa mchezaji wa kutumainiwa. Msimu huu ameongeza maksi zaidi katika kipindi chake cha uchezaji.

**JE, WAJUA?**

MABAO mawili aliyofunga mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Leicester juzi, yamemfanya kwa mara ya kwanza kuweza kufunga katika mechi tatu mfululizo tangu aanze kucheza soka.



# MICHEZO

## NJE YA UWANJA



## MESSI ALIVYOTUPIA HAT-TRICK YA 50

**MARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameelezewa kama mchezaji mkubwa zaidi duniani na kocha wake Ernesto Valverde baada ya kutupia mabao matatu ['hat-trick'] na kuisaidia Barcelona kutokea nyuma mara mbili na kuichapa Sevilla 4-2 Jumamosi.

Messi alisawazisha bao la kwanza la Jesus Navas na kisha la Gabriel Mercado kabla ya kuendelea kutupia na kukamilisha hat-trick yake hiyo ikiwa ni ya 50 katika wasifu wake kisoka.

Luis Suarez alikamilisha karamu hiyo kwa kutupia bao la nne na hivyo kuwafanya mabingwa hao watetezi kukaa kileleni mwa La Liga kwa pointi 10 zaidi, lakini alikuwa ni Messi aliyejizolea sifa lukuki.

"Lionel si yeye pekee aliyefunga mabao matatu, lakini unapaswa kuona wapi, lini na namna alivyoyapata," Valverde aliwaambia wanahabari.

"Tuna mchezaji anayeamua na mzuri.

"Timu zote zina wachezaji wanaoamua, lakini tunaye bora duniani. Na si tu kwa mabao yake, lakini kwa sababu [mara zote] anaonekana katika eneo sahihi kwa wakati sahihi."



Straika wa Simba, Meddie Kagere, akijaribu kumlamba chenga beki wa Azam FC Yakubu Mohamed kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hizo mbili Uwanja wa Taifa wiki iliyopita.

# USIYOYAJUA SIMBA VS AZAM FC TAIFA

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya Meddie Kagere na moja la John Bocco yameifanya timu ya Simba kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kiungo wa zamani wa Yanga, Frank Domayo, aliifungia Azam bao la kufutia machozi kwenye mechi hiyo iliyopigwa Ijumaa.

Ni mechi ambayo imeiwezesha Simba kufikisha pointi 45 kati ya mechi 18 ilizocheza, ikiendelea kujikita kwenye nafasi ya tatu, lakini kuisaka nafasi ya kwanza inayoshikiliwa kwa muda mrefu na mahasimu wa jadi Yanga yenye pointi 61 kwa mechi 25 ilizocheza.

Kwa upande wa Azam imebakiwa na pointi zake 50 ikiwa pia imebaki kwenye nafasi yake ya pili, ikicheza mechi 25.

Hata hivyo, kuna mengi yasiyojulikana yaliyoizunguka mechi hiyo...

**1. Msimu wa 11, Simba bado mbabe**

Ilikuwa ni mechi ya 21 kati ya timu hizo mbili tangu zilipoanza kukutana kwa mara ya kwanza msimu wa 2008/09, ikiwa pia ni msimu wa 11 kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ushindi wa mabao 3-1, umeifanya Simba kuendeleza rekodi nzuri kwenye mechi za Ligi Kuu kwa kuifunga Azam mara 10.

Kati ya mechi 21 zilizokutana kwenye mechi za ligi, Simba imeshinda kwa idadi hiyo ya mechi, Azam ikishinda mara tano na zikitoka sare mara sita.

**2. Bocco kuwafunga waajiri wake wa zamani**

Bao lililofungwa na Bocco lilimfanya mchezaji huyo kuwafunga waajiri wake wa zamani, Azam FC. Ndiyo maana straika huyo ambaye anaichezea Simba kwa msimu wa pili sasa, hakushangilia bao hilo zaidi ya kufurahi tu kawaida. Bocco anaifunga Azam kwa mara ya kwanza tangu alipoihama timu hiyo 2017.

Straika huyo ndiye aliyefunga bao pekee mwaka 2007 lililoipandisha Azam FC kwenye Ligi Daraja la Kwanza na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/09. Ameichezea Azam kwa misimu tisa ya Ligi Kuu tangu ilipomsajili kutoka Cosmopolitan.

**3. Watatu wamezichezea timu zote mbili**

Katika mechi hiyo kulikuwa na wachezaji watatu waliowahi kuzichezea timu zote mbili. Wachezaji hao walikuwa wakicheza dhidi ya timu zao za zamani.

Bocco aliichezea Azam FC tangu ikiwa Daraja la Kwanza na kuichezea kwa misimu tisa kwenye Ligi Kuu, kabla ya kujiunga na Simba.

Wa pili ni Aishi Manula alisimama langoni kwa upande wa Simba. Huyu aliichezea Azam FC kuanzia mwaka 2012, akisajiliwa kama kipa wa kikosi cha pili, lakini baadaye akawa kipa namba moja wa kikosi cha kwanza, kabla ya kuhamia Simba mwaka 2017.

Mchezaji wa tatu ni Ramadhani Singano 'Messi'. Winga huyu alikuwa kwenye kikosi cha vijana wa Simba, kabla ya kupandishwa kwenye kikosi cha kwanza na aliyekuwa Kocha Mkuu wakati huo Patrick Liewig ambaye alipandisha wachezaji wengi msimu huo na kuachana na wakongwe. Kwenye mechi hiyo aliichezea Azam dhidi ya timu yake ya zamani, Simba.

**4. Wachezaji wawili majeruhi**

Idadi ya wachezaji waliowahi kuzichezea timu hizo ingeweza kuongeza na kufikia watano kama wachezaji wawili Shomari Kapombe na Erasto Nyoni wasingekuwa majeruhi.

Wachezaji hao wa Simba ambao nao wametokea Azam FC wamepata bahati mbaya kwani wote wawili ni majeruhi kwa kuumia kila mmoja kwa nyakati tofauti na kuikosa mechi hiyo dhidi ya mabosi wao wa zamani.

Kapombe ambaye yeye alianzia Simba, akaenda Azam na kurejea tena Simba aliumia Novemba mwaka jana akiwa mazoezini kwenye kikosi cha Taifa Stars, huku Nyoni akiumia mwanzoni mwa mwaka huu kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar.

**5. Wageni waiteka mechi**

Kwenye mechi hiyo kulikuwa na wachezaji wa kigeni 14 waliocheza mechi hiyo, Azam ikitia fora kwa kuchezesha wanane, Simba ikichezesha sita.

Wachezaji sita wa Simba kutoka nje ni Zana Coulibaly, raia wa Burkina Faso, Paschal Wawa(Ivory Coast), James Kotei (Ghana), Clatous Chama (Zambia), Meddie Kagere (Rwanda) na Emmanuel Okwi (Uganda).

Azam yenyewe ilichezesha wageni wanane ambao ni Razak Abalora, Yakubu Mohammed wote kutoka nchini Ghana, Tafadzwa Kutinyu, Bruce Kangwa na Donald Ngoma (Wazimbabwe), Obrey Chirwa (Zambia) na Nicolaus Wadada (Uganda).

# Wa5 ‘wanaonuka’ katika klabu zao



Ozil

Sanchez

Bale

Isco

Coutinho

**LONDON,** England

NI vigumu kwa wanasoka kusukuma vipaji vyao kufikia kwenye daraja la juu, lakini ni vigumu zaidi kwa wao kubakia kwenye kiwango cha juu katika maisha yao ya soka. Hii ni kwa sababu mambo yanabadilika haraka kwenye soka, suala la kubakia juu ni mapambano ya kila siku.

Kuna nyota wengi Ulaya kwa sasa wanapitia kwenye wakati mgumu zaidi katika maisha yao ya uchezaji. Baada ya wao wenyewe kutengeneza majina makubwa kwa kuonyesha kiwango cha juu, wachezaji hawa sasa wanajikuta kwenye wakati mgumu kutokana na kuwa na kiwango duni.

Pindi akiwa mchezaji ambaye anapendwa zaidi na mashabiki, lakini akajikuta kiwango chake kimeporomoka, analazimika kuondoka kwenye klabu yake. Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao viwango vyao vimeshuka na wanalazimika kuondoka katika klabu zao:

**5. Mesut Ozil**

Kuna nyota wengi wapo kwenye wakati mgumu Ulaya kwa sasa na mmoja wao ambaye yupo katika hali hiyo ni kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil. Mchezaji huyu wa zamani wa timu ya Taifa ya Ujerumani amejikuta kwenye msimu mgumu zaidi hadi sasa, akionekana kushuka kiwango chake.

Ozil alijiunga na ‘Washika Bunduki’ hao akitokea Real Madrid wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2013 na alikuwa katika kiwango cha juu zaidi kwa kipindi cha miaka yake miwili ya mwanzo hapo katika dimba la Emirates, akimaliza kama kiungo mbunifu zaidi katika ligi tano za Ulaya kwa msimu wa 2015/2016.

Hata hivyo, baada ya kuwa na maisha ya kuvutia kwa klabu hiyo ya kaskazini mwa jiji la London, mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid alianza kushuka kiwango miaka miwili iliyopita, na wakati mgumu zaidi umemkuta chini ya kocha, Unai Emery msimu huu.

Kocha huyo amekataa kumuweka kwenye mipango yake katika wiki za hivi karibuni na kwamba amemuonyesha wazi kuwa hamhitaji. Na matokeo yake ni kwamba, Ozil anaweza kulazimika kuondoka hapo Uwanja wa Emirates haraka zaidi huku klabu za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ikiwamo Inter Milan wakitumaini kupata saini yake.

**4. Alexis Sanchez**

Mambo yanaweza kugeuka juu chini haraka zaidi kwenye soka, kama ilivyo kwa winga wa Manchester United, Alexis Sanchez. Nyota huyu wa kimataifa wa Chile alikuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya England wakati akiwa na Arsenal kabla ya kuhamia pale Manchester.

Mengi yaliratajiwa kutoka kwake mshambuliaji huyo wa zamani wa Barcelona wakati akijiunga na ‘Mashetani Wekundu’ hao kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari mwaka jana, lakini Sanchez ameshindwa kufikia matarajio hayo, huku maisha yake ya soka hapo Old Trafford yakionekana kuwa kwenye wakati mgumu.

Sanchez amefunga mabao matano tu na kutoa pasi za mwisho tisa kwa jina lake katika mechi 38 za Ligi Kuu alizocheza kwenye mashindano yote tangu alipojiunga na timu hiyo Januari 2018.

Wakati wengi walikuwa wakimnyoshea kidole Jose Mourinho kwa mbinu zake na ndio sababu ya Sanchez kuwa kwenye wakati mgumu, mshambuliaji huyo ameshindwa kuthibitisha uwezo wake chini ya Ole Gunnar Solksjaer.

Kiukweli wachezaji kama Marcus Rashford, Jesse Lingard na Anthony Martial wote wanaonekana kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi, na Sanchez anaweza kulazimika kuondoka hapo Old Trafford haraka.

**3. Isco**

Mchezaji mwingine ambaye yupo kwenye wakati mgumu kwa sasa ni nyota wa Real Madrid, Isco, mchezaji ambaye yupo kwenye kiwango cha juu kwa kipaji chake na akili ya mpira.

Likija suala la kuwaangalia viungo bora barani Ulaya kwa wakati huu, mchezaji huyu wa kimataifa wa Hispania yupo kwenye kiwango cha juu zaidi. Hata hivyo, kiwango pekee hakitoshi kumfanya mchezaji kuwa kwenye kiwango cha juu na hilo ndilo linalotokea kwa Isco kwa kipindi cha miezi michache iliyopita.

Mchezaji huyo yupo kwenye wakati mgumu hapo katika dimba la Santiago Bernabeu msimu huu. Alikuwa mchezaji anayeanza mara kwa mara katika kikosi cha Julen Lopetegui, lakini ameshindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza baada ya Santiago Solari kuchukua mikoba.

Haaminiwi na kocha kama ambavyo wachezaji wengine wanavyomchukulia. Kwa wakati huu kuondoka kwa miamba hao wa Hispania ni jambo muhimu zaidi kwake. Kama akiamua kuondoka, kuna klabu nyingi zinazomuwania kama vile Manchester City, Barcelona na Paris Saint Germain.

**2. Gareth Bale**

Mchezaji mwingine wa Real Madrid ambaye yupo kwenye wakati mgumu ni nyota huyu wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale. Yeye ni mmoja wa nyota kadhaa wa Ulaya ambao wapo kwenye wakati mgumu zaidi Ulaya kwa sasa.

Macho yote yapo kwa mchezaji huyu wa zamani wa Tottenham Hotspur kwamba anatakiwa kuongoza safu ya ushambuliaji hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo ambaye amejiunga na Juventus wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini ameshindwa kufikia matarajio ya wengi.

Ingawa mshambuliaji huyo amefunga mabao tisa katika mashindano yote msimu huu, hajawa kwenye kiwango cha kuibeba klabu hiyo hasa kutokana na kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

Huku wachezaji vijana kama Vinicius Junior na Lucas Vazquez wakichomoza, raia huyo wa Wales atalazimika kuangalia majaliwa yake ya baadaye haraka iwezekanavyo.

**1. Philippe Coutinho**


Si habari tena kwamba kiungo mshambuliaji wa Brazil, Philippe Coutinho yupo kwenye wakati mgumu pale Barcelona. Amekuwa akijaribu kurudi kwenye kiwango chake, lakini mambo yanaonekana kuwa magumu zaidi kwake.

Mchezaji huyu alitawala vichwa vya habari wakati akiondoka Liverpool kwenda Barcelona kipindi cha majira ya joto mwaka 2018. Alifunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho sita kwa ‘Blaugrana’ hao katika mechi 22 alizocheza kipindi cha pili cha msimu uliopita. Coutinho aliibua matarajio mengi wakati akijiunga na miamba hao wa Catalunya.

Hata hivyo, kwa sasa ndoto yake ya kutamba na klabu hiyo imebakia kuwa jinamizi, kwani kiwango chake kimeshuka na ameshindwa kabisa kujiimarisha yeye mwenyewe. Raia huyu wa Brazil amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 33 alizocheza msimu huu. Na matokeo yake amejikuta akipoteza namba kwa Ousmane Dembele na sasa mashabiki wameonyesha wazi kuwa hawamhitaji tena na atalazimika kuondoka.

## NUKUU


“Baadhi wanasema unahodha hauna maana, lakini kwa Mauro [Icardi] ni kama kuchukua mguu wake kuliko mkono. Anavaa jezi na sifa ya kitambaa hicho na kama kulikuwa na maamuzi ambayo yangepatikana katika siku za nyuma kuhusu pesa au mapenzi ya jezi, yeye huchagua jezi daima,” **mke wa Mauro Icardi, Wanda Nara, ambaye pia ni wakala wake akizungumzia kuhusu mumewe alivyoumia kunyang’anywa unahodha Inter Milan.**



“Kwenda ugenini pale [Allianz Arena], tunajua ni kwa namna gani walivyo wazuri kama timu, tunajua itakuwa vigumu, lakini tunao uzoefu kwenye Ligi ya Mabingwa na ninahisi kama tunaweza kwenda pale na kuwajeruhi,” **kiungo wa kati na nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson, aliiambia BT Sport mara baada ya kutoka sare tasa na Bayern Munich kwenye mechi ya hatua ya 16-Bora Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Anfield Jumanne iliyopita.**



“Fainali kuchezwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani ni hamasa kubwa zaidi kwa wachezaji wote wa Atletico, mara zote kunakuwa na mwitiko mkubwa wa mashabiki na hicho ndicho tunachokihitaji,” **Antoine Griezmann akizungumzia namna wanavyohamasika kupigania kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo msimu huu itachezwa katika uwanja wao wa Wanda Metropolitano**



# MAKAMBO, KAGERE VITA KIATU CHA DHAHABU



Makambo

Na Adam Fungamwango

WAKATI kukiwa na vita kati ya timu zinazosaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambazo ni Simba, Yanga na Azam FC, lakini upande wa pili hivi sasa kumezuka vita nyingine ya kuwania kiatu cha ufungaji wa ligi hiyo.

Pamoja na kwamba wachezaji wengi wanafunga mabao kwenye mechi zinazoendelea za Ligi Kuu, lakini kuna baadhi wanaonekana wako moto wakifunga mechi hadi mechi, lakini pia viwango vyao kwa wakati huu vikiwa juu.

Yeyote yule anaweza kutwaa Kiatu cha Dhahabu, lakini kati ya wachezaji hawa watano ndiyo wanaotarajiwa kwa kiasi kikubwa mmoja wapo kuchukua tuzo ya ufungaji bora na kutwaa tuzo hiyo.

**1. Salum Aiyee (Mwadui)-mabao 13**

Straika huyu wa Mwadui FC, amewashangaza mashabiki wengi wa soka nchini kwa kuwa kinara wa ufungaji kwenye Ligi Kuu mpaka sasa akiwa ameshatupia mara 13.

Kinachowashangaza wengi ni kwamba ni straika mgeni kwenye ligi ya Bongo na si kati ya wale waliozoeleka, lakini amekuwa na idadi nzuri ya kuifungia timu yake mabao, huku akiwapelekesha puta mastraika wa kigeni.

"Siri ni kumsikiliza mwalimu anasema nini na mimi mwenyewe kujiwekea malengo uwanjani. Ni kwamba ninapopata nafasi huwa nakuwa makini kuitumia kwa sababu wakati mwingine huwa hazipatikani kwa urahisi," alisema.

Straika huyo pia ndiye anashikilia rekodi ya kufunga bao la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alifanya hivyo Agosti 22 kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba kwenye moja kati ya mechi za ufunguzi wa Ligi Kuu, alipofunga katika dakika ya tisa, Mwadui ikifungwa mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar na kuwa bao la kwanza kwa msimu huu.

**2. Heritier Makambo (Yanga)-mabao 12**

Baada ya kufunga bao kwenye mechi dhidi ya Mbao FC, Makambo amefikisha jumla ya mabao 12, akiwa nyuma ya kinara Salum Aiyee wa Mwadui FC.

Straika huyo wa Yanga raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, amekuwa msaada mkubwa kwa timu yake kwani kati ya mabao 33 ambayo yamefungwa, yeye amechangia robo nzima.

Ni mmoja wa mastraika wanaotarajiwa kutwaa Kiatu cha Dhahabu kama ataendelea na uwezo wake huo wa kuweka mipira ndani ya kamba.

**3. Meddie Kagere (Simba)-mabao 11**

Ijumaa iliyopita alitangaza hali ya hatari kwa kupachika mabao mawili kwenye mechi dhidi ya Azam FC na kufanikiwa kufikisha jumla ya mabao 11.

Ni pungufu ya mawili tu kumfikia kinara Aiyee. Kagere anaweza kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa sababu si tu kwamba amekuwa na uwezo mkubwa wa kufunga, tena kwenye mechi ngumu, lakini pia timu yake ina idadi ndogo ya mechi ilizocheza, hivyo ana michezo mingi zaidi ya kufunga mabao kuliko wenzake.

**4. Said Dilunga (Ruvu Shooting)-mabao 10**

Ni straika tegemeo kwa Ruvu Shooting kwa sasa. Ameshapachika mabao 10 na kumfanya kukamata nafasi ya nne kwenye kinyang'anyiro cha kusaka Kiatu cha Dhahabu, akiwa sawa na Eliud Ambokile, lakini mwenzake huyo kwa sasa ameshaondoka kwenye ligi ya Tanzania na kuhamia Afrika Kusini kwenye klabu ya Black Leopards FC.

Dilunga naye si wa kubeza, kwani anaweza kupindua meza kibabe na kuwa mfungaji bora kama atandelea kuwa kwenye fomu kama alivyonayo sasa.

**5. Dickson Ambundo (Alliance)-mabao 9**


Ambundo naye ni mmoja wa mastraika aliyewashangaza wengi kwani amepachika mabao tisa, akiichezea timu iliyopanda Ligi Kuu msimu huu Alliance. Wengi wanajiuliza kama angekuwa anaichezea timu zenye majina makubwa ingekuwaje.

Ni straika ambaye kwa sasa anaibeba sana timu yake kutoka kushika nafasi ya mwisho kwenye mzunguko wa kwanza, hadi kuwa timu tishio na iliyo kwenye nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu.

Akiepuka majeraha na kuwa kwenye kiwango kizuri anaweza kutwaa ufungaji bora.

**NAJUA WAJUA**

JONNY Evans wa Leicester, amekuwa mchezaji wa nne kutoka Ireland kufikisha mechi 250 Ligi Kuu England (pia Aaron Hughes, Chris Brunt na Steven Davis) waliweza kufikisha idadi hiyo.



**MAKALA**



# SABABU 3 KWA NINI SARRI ANAPASWA KUTIMULIWA

**LONDON,** England

MAMBO yamekuwa tofauti kabisa na matarajio ya wengi kwa Chelsea na sasa ni wazi kwamba wengi hawana imani na kocha wao. Maneno ya kejeli kutoka kwa mashabiki kama vile "hujui unachokifanya" na "utafukuzwa asubuhi" yalivuma katika dimba la Stamford bridge wakati wakifungwa 2-0 na Manchester United.

Mambo yanabadilika haraka zaidi, kwani mashabiki wa Chelsea hivi sasa wamekuwa kwenye wakati wa kuumizwa zaidi.

Kipigo kutoka kwa Tottenham katika dimba la Wembley kilikuwa cha kwanza kwa Chelsea msimu huu na ndicho kilichoanza kuleta matatizo. Kuanzia hapo wakajikuta wakifungwa na Leicester City, Wolves, Arsenal, Bournemouth na Manchester United.

Inaonekana kwamba mbinu anazozitumia kocha huyu raia wa Italia haziwezi kuiokoa Chelsea kwa vipigo. Hata hivyo, ishara zinaonyesha kwamba mbinu za Sarri sio za kishindani kwa timu na kujikuta wakiwa na matokeo mabaya kwenye Ligi Kuu.

Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini Maurizio Sarri anatakiwa kufukuzwa Chelsea akiwa hajatimiza hata mwaka mmoja kwenye kazi yake...

**1. Ukorofi wa Sarri**

Sarri amejipambanua kuwa kocha mtata zaidi. Anaonekana kutoziamini mbinu zake, na falsafa yake na hajali matokeo ya timu.

Kwa kocha mkubwa kama yeye inaweza kuwa muhimu kwake. Lakini kama haziamini mbinu zake na falsafa zake, hivyo ni vigumu kuwashawishi wachezaji kufanya kile kinachotakiwa dimbani.

Hata hivyo, kocha wa Ligi Kuu hatakiwi kukosa mbinu binafsi za kuwapa hamasa wachezaji wake. Kwenye ligi ya kishindani kama Ligi Kuu ya England, kocha anatakiwa kuwa mtu ambaye anabadilisha mbinu zake mara kwa mara kulingana na mchezo uliopo mbele yake.

Sarri amekuwa na imani kubwa na mfumo wake wa 4-3-3 huku akimtumia zaidi Jorginho kama kiungo mchezeshaji kwenye timu yake kwa muda mwingi. Hataki kubadilika kabisa.

**2. Sarri anatabirika**

Kutabirika kwa Chelsea ya Sarri ni jambo rahisi. Ni kitu rahisi kwa shabiki wa EPL kuweza kutabiri angalau wachezaji nane watakaoanza kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea kwenye mchezo unaofuata. Hivyo hata mbinu zake zinatabirika kwamba atachezesha timu kwa staili gani.

Staili ya uchezaji pia inatabirika kirahisi kwa makocha wake wa timu pinzani. Kipigo chao kutoka kwa Tottenham kilionyesha kwamba Chelsea ilikuwa na safu ya kiungo iliyoshindwa ikiongozwa na Jorginho na beki David Luiz, na ni wazi kwamba makocha wengi wameliona hilo na wanajua namna ambavyo timu yake inacheza. Lakini yeye Sarri ameendelea kuwa muumini wa mbinu ile ile.

Hata mabadiliko anayofanya Sarri kwa wachezaji yanatabirika kirahisi tu. Kwa shabiki yeyote wa Chelsea anayetazama mara kwa mara mechi za timu yake anajua kwamba, Willian anabadilishana na Pedro na Barkley anabadilishana na Kovacic.

Chelsea ya Sarri imeanza na kumaliza kwenye kila mchezo wa mashindano yote kwa mfumo mmoja wa 4-3-3.

**3. Sarri anaongeza matatizo kwa wachezaji**

"Inaonyesha wazi kwamba wachezaji wangu wanacheza bila hamasa na hawana morali kabisa, kiakili wanaonekana hawapo uwanjani kabisa. Sina furaha kwa sababu napenda kuja kwenye vyumba vya kuadilishia nguo kuzungumza kuhusu mbinu za mchezo kwa nini tumepoteza, lakini sasa kundi langu la wachezaji linaonekana wazi kuwa halina hamasa na linacheza bila kuwa na morali ya mchezo."

Hayo yalikuwa ni maneno ya Sarri baada ya Chelsea kufungwa na Arsenal, na Muitaliano huyo alisema kwamba wachezaji wake walikuwa hawana hamasa na ilikuwa vigumu kuwapa morali. Kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Bournemouth pia kilifuatiwa na maneno kama hayo kwamba wachezaji wake hawachezi kwa morali.


Kauli kama hii ni wazi kwamba haiwezi kumhamasisha mchezaji yeyote na pia alirudia wakati walipokumbana na kipigo pale kwenye dimba la Etihad kutoka kwa Manchester City.


Kocha huyu wa zamani wa Napoli pia anaonekana kutokuwa na mahusiano mazuri na kiungo wake Hazard. Amekuwa akimuelezea mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kama ni nahodha na sio kiongozi na alisema nyota huyo anaweza kuondoka kama akitaka. Wachezaji wengi wemeichukulia kauli hiyo kama sio rafiki kwao.

Kumshambulia mchezaji kama Hazard linaweza kuwa sio jambo nzuri kwa Sarri mwenyewe pamoja na wachezaji wake. Kwani kile kiichomtokea Mourinho pale Manchester United ndicho kinachoweza kumtokea yeye kwa kushindwa kuwa na mahusiano mazuri na wachezaji wake.

**NDANI YA 18**

KYLIAN Mbappe wa PSG, amekuwa mchezaji wa kwanza Mfaransa kuweza kufunga mabao 19 katika mechi zake 18 za kwanza za msimu wa Ligue 1 kwa kipindi cha miaka 45 iliyopita.





NI vigumu kwa wanasoka kusukuma vipaji vyao kufikia kwenye daraja la juu, lakini ni vigumu zaidi kwa wao kubakia kwenye kiwango cha juu katika maisha yao ya soka. Hii ni kwa sababu mambo yanabadilika haraka kwenye soka, suala la kubakia juu ni mapambano ya kila siku.

**Uk. 16-17**




Manolas

# WACHEZAJI WA5 EMERY ANAOTAKIWA KUWASAJILI

**LONDON,** England

ARSENAL ilianza msimu kwa matumaini makubwa na ilionekana wazi kuwa ingeweza kuwa kwenye nne-bora na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. Hata hivyo, mambo yalianza kubadikika Novemba, wamekuwa na wakati mgumu wa kufunga kwenye kipindi cha kwanza.

Na hilo limewafanya kupoteza pointi nyingi na kuwa na kiwango duni. Hata hivyo, wameimarika chini ya kocha Unai Emery na bado wanaweza kumaliza kwenye nne-bora kama wakipambana zaidi.

Nafasi pekee ya msimu huu kupata taji ni kwenye Ligi ya Europa ambapo wameungana na Chelsea kwenye hatua ya mtoano ya timu 16. Hilo ndio taji pekee ambalo wapo na pengine wanaweza kuonyesha maajabu yao kwa kulitwaa.

Ukiangalia msimu ujao, mambo yanaweza kuwa tofautu kabisa. Unai Emery atakuwa na nafasi ya kuimarisha wachezaji wake kuweza kuizoea Ligi Kuu ya England. Hata hivyo, ili aweze kufanikisha mipango yake ni lazima asajili wachezaji wapya kwenye dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

Inatarajiwa kwamba Unai Emery atapewa bajeti ya pauni milioni 100 kwa ajili ya kufanya usajili wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kuwasajili wakati wa kipindi cha majira ya joto, ili kuwasaidia kuimarisha kikosi cha kwanza.

**5. Jadon Sancho**

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City amejiimarisha mwenyewe msimu huu akiwa pale Borussia Dortmund. Pia alipata nafasi ya kuanza kuichezea timu ya Taifa ya England Oktoba 12, mwaka 2018 dhidi ya Croatia. Kwa klabu amekuwa na mafanikio ya kuvutia, amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho tisa kwenye mashindano yote msimu huu.

Anaweza pia kushinda taji lake la kwanza akiwa na Borussia Dortmund, ambao kwa sasa wanaongoza kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. Dortmund kwa sasa wanataka dau la pauni milioni 90 kwa ajili ya kumuachia Jadon Sancho, ambapo itakuwa na faida kubwa kwao baada ya kumnunua kwa pauni milioni nane mwaka 2017. Hata hivyo, haijulikani kama Arsenal wataweza kulipa kiasi hicho kwa Sancho.

**4. Nicolas Pepe**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 23 kwa sasa anacheza katika Klabu ya Lille na amekuwa akiwaniwa na timu kadhaa baada ya kufunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu huu.

Kwa uhakika anathamani kubwa pale Lille, lakini ni wazi kwamba hana maisha marefu pale, kwani klabu nyingi zimekuwa zikihitaji huduma yake. Bayern Munich pia imeripotiwa kuwa inataka kumsajili Nicolas Pepe na Arsenal wanatakiwa kufanya haraka kuipata saini yake.

Katika umri wake wa miaka 23, atakuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Unai Emery kumsajili, hasa ikizingatiwa na ukweli kwamba Arsenal wanaukosefu wa winga wakiwa wanamtegemea Alex Iwobi pekee.

**3. Ben Chilwell**

Ben Chilwell amekuwa na msimu mzuri na ameweza kumshawishi Gareth Southgate kumpa nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England, na ameonekana kuimarika zaidi. Na ni wazi kwamba inaonyesha atakuwa kwenye kikosi cha England kwenye michuano ya Euro 2020, hasa ikizingatiwa kiwango alichonacho kwa sasa.

Unai Emery atatakiwa kumsajili kwa sababu Nacho Monreal katika umri wake wa miaka 32 anaelekea mwisho hapo Arsenal. Sead Kolasanic pia haonekani kufiti kwenye staili ya uchezaji ya Unai Emery, Chilwell ndio anaweza kuwa usajili sahihi kwake.

Inaonyesha wazi kwamba Leicester City hawataweza kumuachia beki huyo wa kushoto bila ya pauni milioni 50.

**2. Kostas Manolas**

Kostas Manolas, katika umri wake wa miaka 27, ana majaliwa mazuri ya baadaye. Manolas ni beki aliyetulia na ndio mtu pekee ambaye Unai Emery anamhitaji kwenye kikosi chake kwa sababu Arsenal imekuwa na matatizo katika safu yake ya ulinzi msimu huu.

Hata hivyo, 'Washika Bunduki' hao watalazimika kupigana kiume kuweza kushindana na Juventus ambao wanaonekana wazi kuwa wanamhitaji Manolas kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi. Inaonesha Manolas atawagharimu Arsenal pauni milioni 50.

**1. Ever Banega**

Emery ana uzoefu mkubwa na Ever Banega. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Banega amecheza mara 200 chini ya kocha huyo wa sasa wa Arsenal na hivyo ataweza kufiti kwake. Banega ameshinda mataji mawili kati ya matatu ya Europa akiwa na Emery na hii inaonyesha wazi kwamba wana mahusiano mazuri.

Mwanzo Arsenal walimtaka kumsajili Banega, na huku Aaron Ramsey akiwa anaondoka kwenye klabu hiyo kipindi cha majira ya joto kwenda kujiunga na Juventus, Banega anaweza kujiunga na klabu hiyo. Hata hivyo, katika umri wake wa miaka 30 bado anaweza kuwa msaada kwa Emery.

**USILOLIJUA**

TANGU kuanza kwa msimu wa 2014-15, hakuna mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi klabu tofauti katika ligi tano kubwa Ulaya kuliko straika wa Crystal Palace, Michy Batshuayi (mabao 5 - Marseille, Chelsea, Borussia Dortmund, Valencia na Crystal Palace).





## Wachimbaji wajitosa katika ujenzi wa shule

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WACHIMBAJI wadogo katika Wilaya ya Chunya na wadau wa elimu wameungana na kuanza ujenzi wa shule ya msingi katika Kata ya Makongorosi, ili kuepukana na changamoto ya watoto kutumikishwa kwenye migodi.

Mwenyekiti wa wachimbaji wa wilaya hiyo, George Mtasha, alisema wameamua kufanya hivyo baada ya kubaini uwapo wa changamoto kubwa ya watoto kutumikishwa katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Mtasha alisema wachimbaji hao wameungana kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha elimu kwa watoto na kwamba watakuwa mstari wa mbele kupinga watoto kutumikishwa kwenye shughuli za madini.

"Wachimbaji tumekuwa tukilalamikiwa kuwa tunawatumikisha watoto kwenye shughuli zetu za uchimbaji wa madini, sasa tumekuja tofauti na mitazamo hiyo kwa kuhakikisha tunachangia kujenga shule," alisema Mtasha.

Aliongeza kuwa katika kata hiyo ya Makongorosi shule za msingi ziko, lakini hazitoshelezi mahitaji ya watoto kutokana na idadi yao kutoendana na ukubwa wa shule na hivyo wameamua kuongeza ili kuondoa kisisngizio cha baadhi ya wazazi. Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjini wa Makongorosi, Linus Mwanitega, alisema ndani ya Kata ya Makongolosi kuna shule za msingi nne, huku mahitaji ikiwa ni shule tano ili kutosheleza mahitaji ya watoto wenye sifa za kuanza shule.

Alisema kitendo cha wachimbaji na wadau wengine kujitoa katika kuchangia ujenzi wa shule hiyo ni kusaidia watoto waliokosa fursa hiyo ya kusoma waanze ili kuweza kuliokoa taifa la kesho.

Alisema licha ya kuwapo kwa ujenzi huo, lakini bado kuna mahitaji makubwa ya shule katika eneo hilo kwa madai kuwa watu wanaongezeka kila siku.

"Ujenzi wa shule hiyo ni chachu kubwa ya kuendeleza ujenzi wa shule zingine kwa kuwa katika kata hii kuna ongezeko kubwa la watoto ambao wanatakiwa waendelee kusoma shule na kupata haki yao ya msingi," alisema Mwanitega. Mwanitega alisema katika Kata ya Makongorosi kuna shule za msingi nne, lakini kutokana na uhitaji uliopo, shule za msingi tano zinahitajika na ndio maana wadau wamejitoa kwa kukabiliana na changamoto hiyo.

# Wananchi wamwagiwa ng'ombe maziwa

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

SHIRIKA la Heifer International Tanzania kupitia mradi wake wa maziwa limegawa ng'ombe wa maziwa 396 kwa wananchi wa Kata ya Igamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, kwa ajili ya kuwainua kiuchumi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kukabidhi ndama 75 kwa wananchi hao, Mkurugenzi Msaidizi wa shirika hilo, Rose Marando, alisema katika awamu ya kwanza shirika hilo liligawa ng'ombe 200 kwa wanufaika wa awali.

Alisema ng'ombe hao ambao wote walikuwa majike, walizaa ndama 196 ambao wameendelea kugawiwa kwa wanufaika wengine kupitia utaratibu wa kutoa zawadi ya ng'ombe kwa mwingine ambaye hakupata.

Alifafanua kuwa wanagawa ng'ombe jike pekee na kwamba endapo ndama aliyezaliwa akawa dume anabaki kuwa mali ya mnufaika wa awali mpaka atakapokuwa amepata jike ndio anagawa kwa mwenzake.

"Kupitia kauli mbiu yetu ya 'toa zawadi kwa mwingine' kila aliyepewa zawadi awali anatakiwa na yeye atoe zawadi kwa mwenzake ili kila mtu apate na tunatamani huu utaratibu uende kizazi hadi kizazi na pengine wilaya zima watu wapate ng'ombe."

"Kila mtu anajua faida ya ng'ombe, tutapata maziwa kwa ajili ya afya za familia zetu, tutauza maziwa na kupata fedha, lakini pia tutapata mbolea kwa ajili ya mashamba yetu na hivyo kuimarisha uchumi wetu," alisema Marando.

Alisema kwa sasa shirika hilo halitoi ng'ombe wapya isipokuwa wananchi wanaendelea kupeana kutoka familia zilizonufaika mwanzo na kwamba mnyororo huo utaendelea hata kwa vizazi vingine.

Hata hivyo, Marando alisema changamoto iliyopo ni baadhi ya wafugaji kutozingatia maelekezo wanayopewa na wataalamu ikiwamo usafi wa mabanda ili kuepuka magonjwa.

Akikabidhi ndama 75 kwa wanufaika wa awamu ya pili, Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Plingo, alisema lengo la Serikali ya Wilaya hiyo ni kufikia ng'ombe 1,000 kwenye vijiji 10 ambavyo vipo kwenye mradi huo.

Alisema mradi huo utasaidia kupunguza tatizo la udumavu na utapiamlo kwa watoto katika tatizo ambalo lilidai ni kubwa katika wilaya yake.

Alimwagiza Ofisa Mifugo wa Wilaya hiyo kuwasainisha mikataba maalumu wanufaika wote na kwamba ambaye ng'ombe wake atakufa kwa uzembe ni lazima alipe ili iwe fundisho kwa wanufaika wengine.

"Mtamba mmoja kwenye taasisi zinazozalisha ng'ombe unapata sio chini ya milioni 1.5 na unapata kwa kusubiria, sasa kwa idadi ya ng'ombe tulioletewa ni ukweli usiopingika kuwa Heifer wametumia fedha nyingi sana," alisema Palingo na kuongeza.

"Sasa nataka mikataba isainiwe kati ya wanufaika wote na ofisa mifugo wa wilaya na mimi nipate nakala, ambaye ng'ombe wake atakufa na wataalamu wakathibitisha kuwa ni kwa uzembe, lazima alipe lakini wakithibitisha kuwa ilikuwa nje ya uwezo wako tutakusamehe," alisisitiza.

Alisema mbali na shirika hilo kugawa ng'ombe hao kwa wananchi, lakini pia lilitoa msaada wa kiwanda kwa ajili ya kuchakata vyakula vya mifugo ili kuwarahisishia wafugaji hao kupata chakula cha mifugo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, John Palingo (kulia mwenye shati jeupe), akimkabidhi mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Shiwinga, ndama wa maziwa ambao wametolewa na Shirika la Heifer International Tanzania kwa ajili ya kuwainua wananchi hao kiuchumi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Osha wawania mafundi kujikinga na vihatarishi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (Osha), umetoa elimu nzito kwa mafundi wa fani mbalimbali mkoani Mbeya, kujikinga na vihatarishi vyote kwenye maeneo yao ya kazi ili kuepuka madhara yanayoweza kuwapata wanapokuwa kazini.

Elimu hiyo ilitolewa na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha nchini, Khadija Mwenda, wakati wa Kongamano la Fundi Smart, jijini Mbeya na kushirikisha mafundi wa fani mbalimbali kwa lengo la kuwaunganisha.

Mwenda alisema ikitokea fundi akapata madhara ya aina yoyote anapokuwa kazini anaweza kushuka kiuchumi kutokana na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya matibabu, huku kazi zake za kumwingizia kipato zikiwa zimekwama.

Vilevile, alisema madhara ya kiafya yanapomtokea fundi anapokuwa kwenye utekelezaji wa majukumu yake, inasababisha kupungua kwa nguvu kazi ya taifa.

"Kuna watu ni mafundi wanaweza kuathiriwa na vumbi na kuna watu wanafanya kazi kwenye sehemu za kelele kama mashineni, sasa wanaweza wakaathirika kutokana na kazi hizo, kelele zinaathiri masikio, sasa sisi tunawapa elimu hii ili muweze kujikinga," alisema Mwenda.

Alisema ili mtu aepuke madhara kwenye kazi zao ni lazima wawe na vifaa vya kujikinga ikiwamo vifaa vya kuzuia vumbi lisiingie puani na mdomoni.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Anthony Mavunde, alisema kongamano hilo litafanyika nchi nzima ili kuwatambua mafundi wote ili watumike kwenye miradi inayotekelezwa na serikali.


Alisema serikali inakusudia kuwarasimisha zaidi ya mafundi 10,000 nchini ili kuwawezesha kufanya kazi kwa uhuru na kuifanya kazi ya ufundi kuwa ajira kama ajira zingine zinazokimbiliwa na wengi.

Aliwapongeza viongozi wa Kampuni ya Fundi Smart kwa kubuni wazo la kuwaunganisha mafundi kwa madai kuwa ni kundi ambalo limesahaulika na kazi zao hazithaminiwi kama ilivyo kwa kazi zingine ambazo ni rasmi.

"Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ambayo inatakiwa kufanywa na nyie, sasa tunakusudia kuwatambua mafundi wote nchini kuanzia fani zao, idadi yao na mahali waliko ili watumike kwenye miradi hiyo," alisema Mavunde.

Aidha, alisema wanakusudia kuwaunganisha mafundi hao kwenye vikundi mbalimbali ambavyo vitasajiliwa ili iwe rahisi kuwasaidia kiuchumi na kuwaongezea nguvu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Fundi Smart, Fredy Helbert, alisema lengo la kuanzisha kongamano hilo ilikuwa ni kuwaunganisha mafundi pamoja na wateja wao ili kurahisisha kazi.





# Uongozi Soko Kuu Dodoma wabanwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, Jemes Yuna, ameutaka uongozi wa Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma kuandaa mifumo bora, ili kuiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake bila kuingiliwa na wafanyabiashara.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na uongozi mpya wa soko hilo na wafanyabiashara wakati wa mkutano mkuu uliofanyika jijini.

Alisema mifumo hiyo itasaidia serikali kutekeleza shughuli zake bila kuwabughudhi wafanyabiashara.

Aliwataka viongozi wa soko hilo wawe na ushirikiano wenye tija na Halmashauri ya Jiji ili wafanyabiashara wajikwamue kiuchumi.

"Viongozi pia mnatakiwa kujiepusha na migogoro ya ninyi kwa ninyi na migongano isiyo lazima, kaeni kwa pamoja kutafuta suluhisho bila ugomvi," alisema.

Makamu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wafanyabiashara Soko la Majengo, Ramadhani Siogopi, alisema watahakikisha wanadumisha uhusiano mwema ili kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Viongozi waliochaguliwa katika mkutano huo ni Mwenyekiti Hamisi Bomu, Makamu Abdallah Diwani, Katibu Eliaman Mollel, Katibu Msaidizi Ramadhani Siogopi, Mtunza Hazina Beatrice Yame na wajumbe watano.

# DC ataka wazazi wachangie elimu

**Na Renatha Msungu, BAHI**

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Mkunda, amewataka wazazi na walezi wilayani humo kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano kwa kuchangia vifaa vya shule, ili kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi.

Mkunda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki baada ya kukabidhiwa msaada wa viti na meza na Benki ya NMB kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Mtitaa wilayani humo.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanaisaidia serikali kuchangia baadhi ya vifaa ili kupunguza changamoto ya uhaba wa vifaa hivyo.

"Mkiambiwa elimu bure, msifikiri kila kitu ni bure. Kuna baadhi ya vifaa wazazi mnatakiwa kuchangia, haiwezekani hata dawati serikali ifanye pekee yake," alisema.

Mkunda alivitaja baadhi ya vifaa vya elimu wanavyotakiwa kuchangia wananchi na jamii kuwa ni madawati, vitabu na madaftari.

Kiongozi huyo wa serikali pia alitoa miezi mitatu kwa wakazi wa Kata ya Mitaa kuhakikisha wanamaliza changamoto ya viti na meza katika shule hiyo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mtitaa, Selemani Mbiaji, aliushukuru uongozi wa NMB kwa msaada uliotoa kwa shule hiyo na kuahidi kuvitunza.

Mbiaji alisema shule hiyo ina wanafunzi 332, lakini ina viti 201, akibainisha kuwa kutokana na msaada wa benki hiyo, sasa wana upungufu wa viti 131.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema vifaa walivyokabidhi kwa shule hiyo, vina thamani ya Sh. milioni 10.

Alisema vifaa hivyo walivyokabidhi kwa shule mbili za Mtitaa na Bahi ni viti na meza 51 pamoja na viti maalum 71 kwa ajili ya maabara za shule hizo.

Mlozi alisema benki hiyo inatoa misaada kwa shule ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhudumia jamii kwa kutenga asilimia moja ya faida inayopata kwa mwaka.

Alisema kuwa mbali na elimu, NMB pia inatoa msaada katika sekta ya afya kwa kununua vifaa muhimu kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali na kusaidia katika majanga na utunzaji wa fedha.

Katika kuhudumia jamii, meneja huyo alisema NMB imefungua matawi zaidi ya 228 nchi nzima na mawakala wa benki hiyo zaidi ya 8,620 katika maeneo mbalimbali ili kuwafikia wananchi kwa karibu.



Rais wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Kanda ya Kati, Twaha Nyange akiwaongoza baadhi ya waumini wa dini hiyo katika zoezi la uchangiaji wa damu siku ya maadhimisho ya Bashir Mwenyezi Mungu ya kukumbuka mwana ajaye ambayo hufanyika kila mwaka Februari 20 iliyofanyika jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Ataka ardhi iliyorasimishwa itumike kwa maendeleo

**Na Paul Mabeja,**
CHAMWINO

MTENDAJI Mkuu wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (Mkurabita), Seraphia Mgembe, amewataka ambao ardhi yao imerasimishwa, kuitumia kujiletea maendeleo.

Mgembe aliyasema hayo juzi katika Kijiji cha Membe wilayani Chamwino wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wananchi na watendaji na ugawaji wa hati za kimila 42.

Alisema ardhi inapopimwa, thamani inaongezeka na ni vyema wananchi wasikimbilie kuuza, badala yake waitumie kujiletea maendeleo kwa kukopa ili kupata mitaji itakayowasaidia kulima kwa tija na kufanya shughuli za maendeleo.

Aliwataka wananchi ambao bado hawajarasimisha ardhi yao, kufanya hivyo ili kuepuka migogoro ya ardhi na kupata ulinzi, hasa kwa wanawake pale mwenza anapofariki dunia. "Ukirasimisha ardhi yako na umiliki ukiwa wenu, ina maana hata kama baba utafariki (dunia), basi mkeo atakuwa salama maana ndugu za mume hawataweza kunyang'anya ardhi hiyo," alisema.

Mgembe pia alitumia fursa hiyo kuhimiza wananchi kuchukua hati zao baada ya kupitishwa malipo ya kisheria ya Sh. 2,700.

"Kuna kipindi tulikuja hapa, tukakutana na malalamiko kuwa kiwango kilichowekwa na halmashauri ni kikubwa, Mkurabita tumezungumza na wenzetu, tumekubaliana gharama ile iliyopo kisheria, hivyo hakikisheni mnachukua hati zenu," alisema.


Mbunge wa Chilonwa, Joel Mwaka, alipongeza hatua za kurasimisha ardhi, akieleza kuwa itaondoa migogoro na kusaidia utunzaji wa mazingira.

Ofisa Mipango wa Wilaya ya Chamwino, Joseph Towo, alisema urasimishaji huo ulifanyika mwaka 2012 katika vijiji vya Membe na Mahama.

Alibainisha kuwa zaidi ya viwanja 2,000 vya Mahama vilipimwa na hati 1,500 kutolewa wakati wa upande wa Kijiji cha Membe hatimiliki 400 zilitolewa na mpaka juzi hati 128 zilikuwa zimeshachukuliwa.

Alisema kuwa kutokana na ongezeko la watu na mabadiliko, kuna haja kufanya uthamini nyingine wa ardhi katika vijiji hivyo.

Awali, akisoma risala ya wakulima, Mtendaji wa Kijiji cha Membe, Amina Mushi, aliomba kurudia kwa upimaji baada ya wengi kutopimiwa ardhi yao.





Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo la kisasa la mikutano la Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Nyumba 5,000 kupigwa dawa ya mbu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya nyumba 5,113 katika shehia 31 za Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, zinatarajiwa kupigwa dawa za kuua mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria ikiwa ni kampeni ya serikali kupambana na ugonjwa huo. Akizindua zoezi hilo la upigaji dawa lililofanyika katika Shehia ya Miwani Mkuu wa Wilaya ya Kati, Mashavu Said Sukwa, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua ili kuona wananchi wake wanaishi wakiwa na afya nzuri pamoja na kutokomeza mbu waenezao malaria. Aliwataka wananchi kushirikiana na wataalamu watakaopiga dawa hiyo kila nyumba kwa sababu baadhi ya wananchi hufunga milango ya nyumba kwa kukataa kupigiwa dawa hiyo.

Alisema wapo baadhi ya wananchi ambao wanafikia hatua ya kuwapa talaka wake zao kwa kukubali kupigwa dawa za malaria katika nyumba zao, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao kwa kuwa malaria husababisha vifo. "Wapo wanaume ambao wanawapa maagizo wake zao kwamba wasifungue milango wapigaji dawa watakapofika na endapo wakifungua watawapa talaka...wanaume kama hawa wakitokea naomba taarifa nipewe haraka sana," alisema.

Alisema atawachukulia hatua dhidi ya wananchi wote ambao watakaidi agizo hilo la kupigiwa dawa nyumba zao kwa kuwa agizo hilo ni lazima na sio hiari.

Ofisa Mipango wa Wilaya ya Kati Unguja, Ali Omar, alisema wilaya hiyo ina mwamko mkubwa kwa wananchi kukubali kupigiwa dawa nyumba zao, jambo ambalo limeleta mafanikio makubwa.

Zoezi la upigaji dawa lilianza juzi katika Shehia ya Uroa, huku likiendelea katika shehia nyingine za wilaya ya kati na mikoa mingine ya Zanzibar.

# Usafi wahimizwa kuepuka kipindupindu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohmed Mahmud, amewataka wananchi kuchukua tahadhari ya kuweka mazingira safi hususan katika njia za kupitia maji ili kujiepusha na athari za magonjwa ya mlipuko, kikiwamo kipindupindu.

Mkuu wa Mkoa huyo aliyasema hayo wakati akizindua wiki ya usafi katika Shehia ya Chuini pamoja na Kihinani huko Bububu Wilaya ya Magharibi A Unguja.

Alisema jamii inapaswa kuhakikisha inaweka mazingira safi hususan katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazotarajiwa kuanza mwezi ujao.

Alisema katika pindi cha mvua kumekuwapo na tabia ya kutuwama kwa maji na kuingia katika makazi ya wananchi kunakosababishwa na kuziba kwa mitaro ya maji.

Alisema mitaro hiyo huziba kutokana na jamii kutupa taka katika mitaro hiyo na kushindwa kufanya usafi, hali inayoweza kuleta athari ya magonjwa mbalimbali.

Aidha, aliwataka wananchi wa shehia hiyo kushirikiana na viongozi wa wilaya kuhakikisha wanasafisha mitaro yote ili mvua zitakapoanza kunyesha zisileta athari kubwa.

"Tulishuhudia katika mwaka 2017 wagonjwa walikuwa wengi wa kipindupindu na hadi kusababisha vifo, kwa hiyo mwaka huu, tujitahidi kuweka mazingira yetu katika hali ya usafi ili kuzinusuru afya zetu," alisema.

Wakati huo huo, mkuu huyo wa mkoa aliwaambia wafanyabiashara wanaofanya biashara ndogo ndogo katika kituo cha daladala cha Kihinani kujiandaa kuondoka katika eneo hilo am alo hawaruhusiwi.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wafanyabiashara wanafanya shughuli zao katika meneo maalum ambayo yatakidhi haja pasipo kuleta athari katika shughuli nyingine.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A, Kaptani Khatib Khamis, alisema katika kila kanda ya Shehia za Bububu zitapangiwa siku maalum kwa ajili ya kufanya usafi, jambo ambalo lina umuhimu mkubwa katika afya za wananchi.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika shehia zao kushiriki zoezi hilo ili kukabiliana na maradhi ya mlipuko.

# Shein aipa CCM siri ushindi 2020

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa iwapo viongozi wa chama hicho wataendelea kuwa karibu na wananchi pamoja na kwenda kuwasikiliza changamoto zinazowakabili, itawafanya wananchi waendelee kukiunga mkono chama hicho na kuendeleza ushindi katika uchaguzi mkuu wa 2020.

Akizungumza na viongozi wa CCM wa Wilaya ya Wete Pemba, aliwataka viongozi wa majimbo wakiwamo wawakilishi na wabunge kwenda kwa wananchi wao ili wajue changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi sambamba na kuwa nao karibu ili kukiimarisha chama chao.

Alieleza kuwa CCM haitamridhia kiongozi wa jimbo ambaye amechaguliwa na wananchi, lakini amekuwa haonekani jimboni na kusahau wajibu wake wa kwenda kuwatumikia wananchi.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na CCM, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwapelekea maendeleo endelevu wananchi wote wa Unguja na Pemba bila ya ubaguzi.

Alieleza kuwa CCM itahakikisha wananchi wote wanapata huduma sawa na ilivyokuwa wakati wa ukoloni.

Dk. Shein aliwataka viongozi wa CCM na serikali kufanya ziara za kuwatembelea wananchi ili kujua matatizo waliyonayo na kuyatafutia ufumbuzi badala ya kukaa ofisini.

Alisema kuwa kuwafuata wananchi na kutatua shida zao ni agizo la CCM, ambalo lilitolewa katika Mkutano Mkuu wa CCM jijini Dodoma ikiwa ni moja ya utekelezaji wa ilani.

Dk. Shein aliwakumbusha viongozi wa CCM kufanya kazi za chama na kuwataka kila mmoja kufanya kazi kwa kuzingatia wadhifa wake ikiwamo kufanya ziara kwa pamoja kati ya viongozi wa CCM na serikali na baadaye kufanya tathmini.

Aidha, Dk. Shein aliwataka viongozi hao kuwabaini watendaji wote ambao hawafanyi kazi zao ipasavyo na wamekuwa wakifanya kazi kwa maslahi yao binafsi.

Alisema kuwa kwenye siasa za vyama vingi hakuna kutishana na wala kutukanana na kuwataka viongozi wa CCM Wilaya ya Wete na Mkoa wa Kaskazini Pemba kufanya kazi zao za kukiimarisha chama chao bila hofu.

HABARI KIMATAIFA

# Mshindi urais Nigeria kutangazwa wiki ijayo

**LAGOS, Nigeria**

WAKATI mchakato wa kuhesabu kura ukiendelea Nigeria, Tume ya Uchaguzi nchini humo (INEC), imesema matokeo ya urais yanatarajiwa kutangazwa kuanzia wiki ijayo.

Matokeo ya uchaguzi huo ulioahirishwa saa chache kabla ya vituo vya kupiga kura havijafunguliwa Jumamosi iliyopita, yanatarajiwa kutolewa mapema wiki ijayo, ambapo mshindi ataiongoza Nigeria katika kipindi cha miaka minne.

Hadi kufikia jana mchana mchakato wa kuhesabu kura za uchaguzi wa urais uliofanyika juzi ulikuwa ukiendelea, huku mchuano mkali ukiendelea kati ya Muhammadu Buhari na Atiku Abubakar.

Hata hivyo, muda mfupi kabla ya vituo vya kupiga kura havijafunguliwa, mwanajeshi mmoja aliuawa na wengine 20 walijeruhiwa baada ya kundi la Boko Haram kuushambulia mji wa Maiduguri, ulioko kaskazini mashariki mwa Nigeria.

Kura hizo zilikuwa zikihesabiwa, huku tume ya uchaguzi ikiwa imeongeza muda wa kupiga kura katika baadhi ya vituo kutokana na kuchelewa kufunguliwa kwa vituo hivyo na baadhi ya mashine za kupigia kura kushindwa kufanya kazi ipasavyo.

Wakizungumza baada ya kupiga kura, Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari na mpinzani wake mkuu mfanyabiashara Atiku Abubakar wote wamesema wana uhakika wa kushinda.

"Hadi sasa mambo ni mazuri. Nitajipongeza mwenyewe. Nitaibuka mshindi," alisema Buhari wakati akizungumza na waandishi habari.

Buhari ambaye anagombea muhula wa pili madarakani, katika kinyang'anyiro hicho cha kuliongoza taifa hilo lenye uchumi mkubwa barani Afrika, amepiga kura katika mji alikozaliwa wa Daura, Jimbo la Kaskazini la Katsina, huku Atiku akipiga kura yake Yola, mji mkuu wa Jimbo la Adamawa.

Ofisa wa ngazi ya juu wa Tume Huru ya Uchaguzi Nigeria, INEC, Festus Okoye, alisema upigaji kura tayari umekamilika kwenye baadhi ya maeneo na hatua ya kuhesabu kura imeshaanza.

Okoye alisema tume hiyo imeongeza muda kwenye baadhi ya vituo vya kupiga kura ambavyo vilichelewa kufunguliwa.

Alibainisha kuwa wanayashughulikia matatizo mbalimbali yaliyojitokeza kama vile dosari katika shughuli nzima ya uchaguzi, ikiwamo masuala ya usalama.

"Tunajaribu kuyashughulikia matatizo haya na tuna uhakika kwamba tutafanikiwa," alisema Okoye.

*DW*




Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, akipiga kura katika mji alikozaliwa wa Daura, Jimbo la Kaskazini la Katsina.
**PICHA: DW**

# Viongozi Congo wasaini kiapo cha utiifu kwa Kabila

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa zamani wa DRC, Joseph Kabila, ambaye alikabidhi madaraka kwa Felix Tshisekedi, amewasainisha viongozi wa muungano wake wa FCC kiapo cha utiifu kwake.

Muungano wa vyama vinavyomuunga mkono Rais Kabila wa Common Front For Congo (FCC), umekuwa wenye nguvu zaidi bungeni, baada ya kupata wingi mkubwa wa viti katika uchaguzi uliofanyika Desemba 30, ambao pia ulimpa ushindi wa urais kiongozi wa upinzani Felix Tshisekedi.

Ni muda wa mwezi mmoja umepita tangu makabidhiano ya mdaraka yafanyike.

Rais mstaafu Kabila alikutana na viongozi wa vyama 18 vinavyounda muungano wake kwenye shamba lake lililoko Kingakati, karibu na Kinshasa.

Ilielezwa kuwa Rais mstaafu Kabila aliwasainisha waraka wa dhamiri wenye nukta muhimu saba.

"Tunasisitiza uaminifu wetu na utiifu wetu kwa Joseph Kabila Kabange, Rais wa heshima wa Jamhuri." Ni sehemu ya kiapo hicho.

Kwenye uchaguzi huo, Chama cha Tshisekedi cha Union for Democracy and Social Progress (UDPS) kilipata viti 32 vya uwakilishi bungeni.

Hadi sasa Rais Tshisekedi bado hajateua waziri mkuu na amekuwa akifanya kazi na timu ya mpito ya serikali ilioachwa na mtangulizi wake.

Viongozi vya vyama vya FCC walioku-tana Jumatano walikubaliana kuubadili muungano huo kutoka ushirika wa uchaguzi na kuufanya kuwa jukwaa la kisiasa la serikali.

Lakini mabadiliko hayo haimaanishi kuwa watapitia upya makubaliano ya kugawana madaraka walioujadili na Tshisekedi.

Msemaji wa serikali na FCC, Lambert Mende, alisema Rais Tshisekedi na Kabila walikuwa na makaribiano ya kiitikadi. Alisema wote walikuwa na mazungumzo juu ya kuunda serikali ya muungano.

Kuchaguliwa kwa Rais Tshisekedi kuwa Rais wa Congo kuliashiria mabadiliko ya kwanza ya amani ya uongozi nchini DRC tangu ilipopata uhuru wake kutoka Ubelgiji mwaka 1960.

Rais Tshisekedi alichukua madaraka kutoka kwa Kabila aliyeiongoza nchi hiyo kwa miaka 18. Mgombea mwingine wa upinzani, Martin Fayulu, anapinga uhalali wa uchaguzi huo.

*DW*

# Saudia yamteua binti mfalme kuwa balozi Marekani

**RIYADH, Saud Arabia**

SAUDI Arabia imemtangaza binti mfalme, Rima bint Bandar al-Saud, kuwa balozi wake nchini Marekani, akiwa mwanamke wa kwanza kuwa balozi wa ufalme huo.

Uteuzi wake ulifanywa juzi hadharani kwa amri ya ufalme huo.

Rima aliishi Washington DC nchini Marekani katika kipindi kirefu cha utoto wake.

Rima anachukua wadhifa huo wakati mgumu, huku Saudia ikijaribu kukabiliana na kashfa ya kimataifa kuhusu mauaji ya mwanahabari, Jamal Khashoggi.

Kabla ya kifo chake, Khashoggi, alikuwa akiliandikia gazeti la The Washington Post, ambapo mara kwa mara alikuwa akiikosoa serikali ya Saudia.

Saudia ilikana kwamba mwanamfalme Mohammed Bin Salman alihusika katika kifo chake madai ambayo idara ya ujasusi nchini Marekani ilitilia shaka.

Hata hivyo, wabunge nchini Marekani wamejaribu kuishinikiza Ikulu ya Whitehouse kuchunguza kisa hicho. Hivi karibuni, wanachama wa bunge la Congress walichunguza uhusiano kati ya Saudia na Marekani katika maeneo mengine, ikiwamo kuhusu teknolojia ya kinyuklia pamoja na vita nchini Yemen.

Rima atachukua jukumu lote la ndugu yake mdogo mwana mfalme Khalid bin Salman, ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ulinzi nchini humo

Pia, anafuata nyayo za baba yake, Bandar bin Sultan al-Saud ambaye alishikilia wadhifa huo wa ubalozi wa Marekani hadi 2005, na alitumia kipindi kirefu cha utoto wake nchini Marekani.

Rima amesomea shahada ya sanaa ya masomo ya kumbukumbu kutoka Chuo Kikuu cha George Washington University.

Tangu kurudi kwake mjini Riyadh 2005, binti mfalme Rima amefanya kazi katika nyanja za kibinafsi na zile za umma.

Ameshikilia nyadhifa tofauti za kibiashara, ikiwamo ile ya ofisa mtendaji mkuu katika kampuni ya Harvey Nichols Riyadh.

Binti mfalme huyo ni mpiganiaji mkuu wa haki za kibinadamu za wanawake katika taifa ambalo linakosolewa kwa rekodi yake ya usawa wa kijinsia.

Hivi karibuni Rima alikuwa akifanya kazi katika halmashauri ya michezo nchini Saudia akiwa na lengo la kuimarisha idadi ya wanawake wanaoshiriki katika michezo. Pia anajulikana kwa kazi yake nzuri katika kampeni dhidi ya saratani ya matiti.

*BBC*

# Skauti wamuenzi Nyerere kwa usafi

**Na Beatrice Philemon**

ZAIDI ya maskauti 300 kutoka shule nne za kimataifa jijini Dar es Salaam, jana walitembelea nyumbani kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kufanya usafi kwenye eneo la ufukwe kwa ajili ya kumuenzi.

Walichukua hatua hiyo kuenzi mchango wake kwa skauti nchini pamoja na kuadhimisha Siku ya Kuzaliwa kwa Mwanzilishi wa Skauti Duniani, Bwana Baden Powel.

Kiongozi wa Skauti, Master Cuthbert Safari, alisema walikwenda kujifunza elimu ya mazingira na kusaidia watoto kujua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira katika sehemu za fukwe, maeno wanayoishi ili watoto wawe mabalozi wa usafi miaka ijayo kwa sababu watu wengi wamesahau suala la mazingira.

"Hii ni mara ya kwanza kushiriki katika zoezi hili, tutakuwa tunafanya zoezi hili la usafi kwenye maeneo tofauti tofauti kila baada ya miezi mitatu," alisema.

"Lengo la zoezi hili ni kudumisha moyo wa kujitolea kwa skauti na vijana kwa ujumla. Vile vile tulitaka mama Maria Nyerere azindue kitabu kinachohusu vijana kiitwacho Mwenendo na Tabia Nzuri kwa kijana kilichoandikwa na Mzee Biga Kaisi," alisema.

Cutherbert alishukuru mfuko wa Rejuvation Fund kwa kuwasaidia kuwapatia vifaa kwa ajili ya usafi na chakula kwa ajili ya wanafunzi walioshiriki katika kampeni hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya familia ya Mwalimu Nyerere, mjukuu wa Mwalimu Nyerere, Moringe Magige, aliwashukuru skauti kwa kufanya usafi katika fukwe nyumbani kwa Mwalimu Nyerere, kumuenzi babu yake kwa mchango wake mkubwa kwa Skauti Tanzania.

"Sisi kama familia, tumefurahi kuwa na nyie siku ya leo na kumtembelea bibi katika eneo lake, bibi yenu ni mzee sana, leo ajisikii vizuri, ameamka anajisikia vibaya kwa hiyo hamtaweza kumwona na hataweza kuzindua kitabu, ila sisi tutawapa ushirikiano wote mnaohitaji ili muweze kusafisha fukwe ya babu yenu na rais wenu," alisema.

Moringe alipokea kopi ya kitabu hicho kwa niaba ya mama Maria Nyerere na aliwaahidi kumkabidhi.

Akizungumza na Nipashe, Carlos Mdemu kutoka Taasisi ya Kijamii ya Masuala ya Mazingira alisema wameamua kushiriki katika kampeni hii ili kuwafundisha watoto nini maana ya usafi katika maeneo yetu, kwa nini ni muhimu kusafisha mazingira yetu , baharini na ni aina gani ya takataka zinazooza na zisizooza.



Katibu wa kikosi kazi cha kuratibu zoezi la serikali kuhamia Dodoma, Meshach Bandawe, akiongea na mafundi katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais linalojengwa katika mji wa Serikali Ihumwa jijini Dodoma, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mji wa serikali. **MPIGAPICHA WETU**

## Sababu wanafunzi jamii ya wafugaji utoro

**Na Salome Kitomari**

WASICHANA 23 kutoka jamii za kifugaji Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, wanadaiwa kutoripoti Shule ya Sekondari ya Oldonyowas kutokana na baadhi yao kuolewa.

Aidha, wavulana 15 kutoka jamii hiyo nao hawajaripoti sekondari kwa kile kinachoelezwa ni kutumiwa na wazazi kwa shughuli za ufugaji na mwamko mdogo wa kupenda elimu wa eneo hilo.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Mbunge wa Viti Maalum mkoani Arusha, Amina Mollel, alipotembelea shule hiyo kujionea maendeleo ya kitaaluma.

Mbunge huyo pia alitembelea shule hiyo kujionea utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kujenga vyumba vya madarasa, kazi iliyofanywa na serikali ya kijiji cha Oldonyowas kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Shule hiyo ina wanafunzi 150 ambao wameanza masomo, iko katika eneo la wafugaji wa jamii ya Kimasai.

Mbunge huyo alisema akiwa shuleni humo alikutana na mtoto wa kidato cha kwanza ambaye ni mjamzito na familia yake ilishapokea mahari ya binti huyo mwenye umri wa miaka 16.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, mwanafunzi huyo alifikishwa shuleni humo kwa ajili ya kutoa maelezo juu ya hali yake, na alithibitisha kuwa ujauzito huo ni wa kijana ambaye wazazi wake wameshapokea mahari.

Akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo, Mollel alikemea tabia ya wazazi kutoka katika jamii ya wafugaji kuachana na tabia ya kuwaozesha binti zao katika umri mdogo na badala yake wawapeleke shule.

"Wazazi ni vyema wakaelewa kuwa ukimwelimisha mtoto wa kike ni sawa na kuielimisha jamii kwa ujumla," alisema.

Aidha, aliipongeza serikali kwa jitihada za elimu bure ambayo imewezesha watoto wengine kupata elimu bure.

Mbunge huyo aliwazawadia wanafunzi hao vifaa vya masomo, huku akiwataka kusoma kwa bidii kwa kutambua kuwa elimu ndiyo msingi wa mafanikio kwenye maisha yao. Alisema kuwa mwaka jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, ilibainika kuwa wanafunzi 41 hawakuripoti kidato cha kwanza kwa sababu mbalimbali, ikiwamo watano kuhamia nchini Kenya na wazazi wao na mmoja kuwa melzi wa familia kwa ajili ya kumuuguza mama yake.

Aidha, katika kikao hicho walikubaliana kuwatafuta watoto hao kujua waliko na halmashauri iliahidi kuwa iwapo watapatikana waterejeshwa shuleni

Kwenye baraza walikubaliana kujua watoto hawa wako wapi na kama wapo walioolewa, na endapo watapatikana na wako tayari kuendelea na masomo wangerejeshwa shuleni.



## Samia apongeza halmashauri mapato

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kutumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa muindombinu ya afya katika hospitali na kituo cha afya cha Kaliua.

Samia amesema hatua hiyo itasaidia kusogea huduma za afya ikiwamo za upasuaji wa wajazito na za mama na mtoto karibu na kuwaepusha wananchi kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hizo katika Wilaya ya Urambo.

Makamu wa Rais alitoa kauli hiyo kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Kolimba wilayani Kaliua ikiwa ni siku nne ya ziara yake mkoani Tabora.

Alisema kitendo cha halmashauri hiyo cha kutenga sehemu ya mapato yake ya ndani kujenga jengo la upasuaji kwenye Kituo cha Afya Kaliua na ununuzi wa vifaa kwa gharama za shilingi milioni 159 na kile cha ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya kwa gharama ya shilingi milioni 352 ni mfano mzuri ambao unakusudia kusogeza huduma karibu na wananchi.

Makamu wa Rais alizitaka halmashauri nyingine nazo kutumia sehemu ya mapato yake ya ndani kuboresha huduma za jamii ikiwamo maji, afya, elimu na barabara ili kuwafanya wananchi kuwa na mazingira mazuri katika uzalishaji.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Dk. John Pima, alisema katika mwaka huu wa fedha wametoa mikopo ya shilingi milioni 207 kwa vikundi 61 ikiwa ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato yake.

Alisema hadi kufika mwisho wa mwaka wanaweza kutoa mikopo kwa vikundi vingi.

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MASHAMBA/VIWANJA**

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**NAFASI ZA KAZI**

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la The Guardian*

*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,*

*au piga simu: 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SANCHEZ: TOTTENHAM BADO INA NAFASI EPL

**LONDON, England**

MCHEZAJI Davinson Sanchez amesisitiza kwamba, Tottenham wamepata kila kitu kuwa miongoni mwa timu zinazowania taji la Ligi Kuu la England msimu huu.

Manchester City na Liverpool kwa sasa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu zote zikiwa zimeipita Spurs kwa pointi tano katika mbio za ubingwa huo, huku Chelsea na Arsenal zikiwa nyuma ya kikosi hicho cha Mauricio Pochettino.

Lakini katika mchezo wa juzi Jumamosi, Spurs ilifungwa 2-1 na Burnley, ila Sanchez anaona kwamba bado wana nafasi.

"Kiukweli timu yoyote inapocheza na sisi inakuwa inatukamia zaidi kwa sababu tupo kwenye nafasi ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu," alisema mara baada ya mchezo huo wa Jumamosi.

"Lakini ni kwamba timu zinacheza na sisi kwa kutuona kwamba tuko imara kwenye mbio za ubingwa, matokeo haya ya kufungwa dhidi ya Burnley sio ya ajabu zaidi kwetu.

"Sisi tumejipanga kutaka kuweka historia kwa sababu tunajua kwamba tuna nafasi ya kufanya hivyo," alisema."

# De Jong ataja sababu kuichagua Barcelona

**AMSTERDAM, Uholanzi**

KIUNGO wa Ajax, Frenkie de Jong, amesema kwamba ana hamu kubwa ya kuungana na mchezaji bora, Lionel Messi pale Barcelona wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alisaini kuwachezea miamba hao wa Katalunya kwa euro milioni 75 wakati wa dirisha dogo la usajili Januari, na atajiunga na timu yake hiyo pale Camp Nou mwanzoni mwa msimu ujao.

Akiwa amejiimarisha kuwa mmoja wa wachezaji bora Ulaya, De Jong ameelezea jinsi anavyojisikia kwenda kucheza Barcelona sambamba na Messi.

Akizungumza na tovuti ya klabu yake, alisema: "Nina hamasa kubwa ya kutaka kucheza pamoja na Messi, nasubiri kwa hamu kubwa mno. Kwa mawazo yangu mimi yeye ni mchezaji bora wa wakati wote.

**"Ni vigumu kumuelezea. Nafikiri yeye ndiye mchezaji aliyekamilika zaidi. Ana uwezo wa ku fanya chochote uwanjani, anatengeneza nafasi nyingi dimbani, mguu wake wa kushoto ni wa maajabu."**

Licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City na miamba wa Ufaransa, Paris Saint-Germain, De Jong aliamua kuichagua Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 aliongeza: "Mara zote nimekuwa na ndoto ya kuichezea Barca tangu nikiwa mdogo. Nilitaka kuichezea Barca. Nawapenda wachezaji wake, napenda staili wanayocheza. Nafikiri Barca ipo kwenye ndoto zangu. Ndoto yangu ni kuja kuwa mchezaji muhimu wa Barcelona, natumaini nitakuwa naanza kwenye kikosi cha kwanza na kushinda mataji mengi na Barcelona."

# Chelsea kukata rufani kuipinga Fifa

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea ambayo imepigwa marufuku na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ya kusajili wachezaji kwa miaka miwili baada ya kukiuka kanuni ya kuwasajili wachezaji wadogo, imesema itakata rufani.

Marufuku hiyo itakayodumu hadi mwaka 2020, haitajumuisha kuwazuilia wachezaji kuhama klabu hiyo na pia haijumuishi timu ya wanawake.

Klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya England sasa imesema itakata rufani kupinga uamuzi huo.

Chelsea pia imepigwa faini ya euro 460,000, huku Chama cha Soka cha England (FA), kikiwatoza faini ya euro pauni 390,000.

Uamuzi huo unafuatia uchunguzi wa Fifa kuhusu Chelsea inavyowasajili wachezaji wa chini ya miaka 18, ikiwa ni pamoja na usajili wa mshambuliaji wa zamani, Bertrand Traore.

Shirikisho hilo la dunia linalosimamia mchezo wa kandanda, limesema kuwa Chelsea imevunja sheria katika usajili wa wachezaji 29 kati ya 92 waliyochunguzwa.

"Tunakubaliana na Fifa kwa kuafiki kuwa hatukuvunja sheria kuhusiana na visa 63 vya usajili wa wachezaji hao, lakini klabu hii imeshangazwa na hatua ya Fifa kukataa maelezo kuhusiana na wachezaji 29 waliosalia," inasema taarifa kutoka klabu hiyo ya Stamford Bridge.

"Chelsea imezingatia kanuni zote na inajiandaa kuwasilisha rufani yake Fifa."

Kwa mujibu wa ufichuzi wa Football Leaks, mtandao wa Ufaransa wa Mediapart ulidai kuwa Novemba usajili wa Chelsea wa wachezaji 19 ulichunguzwa katika uchunguzi huo wa miaka mitatu.

Mediapart unadai kuwa wachezaji 14 waliyosajiliwa walikuwa chini ya miaka 18.

Mara ya kwanza kuripotiwa kuwa Chelsea inachunguzwa ilikuwa Septemba mwaka 2017.

Mchezaji wa kimataifa wa Burkino Faso Bertrand Traore - ambaye sasa anachezea klabu ya Lyon inayoshiriki Ligue 1 - alitia saini mkataba wa Chelsea mwaka 2013 akiwa na miaka 18, lakini hakusajiliwa hadi Januari mwaka 2014.

Mediapart unaripoti kuwa Fifa ina ushahidi kuwa Chelsea ilidanganya kuhusiana na tarehe ya usajili huo, baada ya kubaini kuwa Traore aliichezea The Blues mara 25 licha ya kwamba hakuwa amesajiliwa na Chama cha Soka cha England.

Chelsea imekiri kuwa ilimlipa mama yake euro 155,000, ikiwa ni pamoja na pauni 13,000 walizomlipia- AJE Bobo-Dioulasso - Aprili mwaka 2011 kukubali awatilie saini mkataba.

Mkataba huo unadaiwa kufikiwa miaka minne na nusu licha ya kuwa sheria inayodhibiti usajili wa wachezaji waliyo chini ya miaka 18 ni miaka mitatu.

# Juve itapindua matokeo kwa Atletico - Allegri



**TURIN, Italia**

JUVENTUS wanauweza wa kufanya kitu kizuri zaidi msimu huu baada ya kutoka kufungwa na Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, amesema kocha wao, Massimiliano Allegri.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, walifungwa 2-0 kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano Jumatano iliyopita, mabao yake yakifungwa na Jose Gimenez na Diego Godin na kuiweka Atletico kwenye nafasi nzuri ya kutinga robo fainali.

Juve imeshinda mara mbili katika mechi zake tano zilizopita kwenye mashindano yote, wakiwa pia wamefungwa 3-0 na Atalanta na kutolewa kwenye michuano ya Coppa Italia.

Hata hivyo, Allegri anaamini kwamba kikosi chake kina uwezo wa kubadilisha matokeo kwenye mchezo wa marudiano dhidi ya Atletico kama watashinda mechi zake tatu za ligi dhidi ya Bologna, Napoli na Udinese.

"Tuna siku 20 za kujiandaa ili kuikabili Atleti," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina uhakika utakuwa usiku mzuri zaidi kwetu. Sijui kama tutafuzu au tutashindwa, tutaona siku hiyo ya Machi 12, lakini tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha tunakuwa bora wakati wa mechi zetu tatu za Serie A."

## LACAZETTE KUKOSA MBILI LIGI YA EUROPA

**LONDON, England**

MCHEZAJI Alexandre Lacazette atakosa mechi zote za Arsenal kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 za Ligi ya Europa baada ya mshambuliaji huyo kupewa adhabu ya kukosa mechi tatu, kufuatia kutolewa nje kwenye mchezo dhidi ya BATE.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja baada ya kumpiga kiwiko Aleksandar Filipovic katika mchezo ambao Arsenal ilifungwa 1-0 na BATE na sasa hatacheza mechi zijazo dhidi ya Rennes.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, tayari ameshatumikia adhabu ya kukosa mchezo mmoja, kwani alikaa nje wakati Arsenal ikishinda 3-0 nyumbani katika Uwanja wa Emirates.

Vijana hao wa kocha, Unai Emery walifuzu hatua ya mtoano wa timu 16 na sasa watacheza na Rennes inayoshiriki Ligi Kuu ya Ufaransa baada ya droo yake kufanyika Ijumaa.

Hivyo inamaana kwamba Lacazette atarudi kuichezea Arsenal kwenye hatua ya robo fainali kama itafuzu, kwani mechi zote mbili atakuwa nje.




# GUARDIOLA: PRESHA HAITAKIWI MAN CITY



**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema Manchester City haistahili kuwa na presha wakati ikizungumzwa kuwa ina nafasi ya kushinda mataji manne msimu huu.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya England, wametinga robo fainali ya Kombe la FA na pia ilifunga Schalke kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora, na sasa City wana nafasi ya kutwaa mataji manne msimu huu.

Hata hivyo, Guardiola amesisitiza kuwa ni mapema mno kuipa nafasi City kuwa na uwezo wa kutwaa mataji manne kwenye mashindano yote inayoshiriki msimu huu.

"Niulize swali hili Aprili au Mei nitakupa jibu lake," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini sasa ni Februari haiwezekani kuzungumzia kuhusu jambo hilo ni mapema zaidi kwa sasa.

"Kevin (De Bruyne) alizungumza vizuri mno kwenye mkutano wake na waandishi wa habari nchini Ujerumani, kwamba malengo yetu ni kuwa tunaangalia mchezo unaofuata. Hivyo kwa sasa hatustahili kuwa na presha na hilo.

"Kwa sasa kuzungumzia uwezekano wa kutwaa mataji manne ni haraka mno, najua kwamba, Sir Alex Ferguson akiwa na Manchester United hakufanya hivyo, ingawa alishinda mataji matatu.

"Hivyo kwetu sisi hatustahili kuwa na presha na hilo, kwani bado ni mapema mno kulizungumzia hilo, sisi kwa sasa tunaangalia zaidi mchezo uliopo mbele yetu."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AWEKA REKODI, ATAMANI KUZIFUNJA ZAIDI

●●● Soka bado ni kufurahia, kufunga mabao na kuvunja rekodi ni kitu kinachonisukuma...

**PARIS, Ufaransa**

Kylian Mbappe amefunga mabao mawili wakati Paris Saint-Germain ikishinda 3-0 dhidi ya Nimes Jumamosi na kuandika rekodi mpya, lakini kocha Thomas Tuchel anahisi mshambuliaji huyo angeweza kufunga angalau mara mbili ya idadi hiyo.

Kwa mabao hayo mawili sasa Mbappe amecheka na nyavu mara 51 kwenye Ligue 1 akiwa hapo Parc des Princes.

Bao lake moja lilikataliwa kwa madai kwamba aliotea, kabla ya shuti lingine kuchezwa na kipa Paul Bernardoni.

Hata hivyo, alipopata nafasi nyingine mbili, ilionekana haikuwa siku ya Mbappe, lakini alifanikiwa kufikisha idadi hiyo ya mabao 51 akiichezea PSG.

Kocha Mkuu wa PSG, Tuchel, alifurahishwa na kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, lakini anaona Mbappe alipashwa kuondoka na mpira kwa kutupia hat-trick.

"Ndiyo [alikuwa vizuri], lakini leo alipaswa kutupia [mabao]manne ama matano," Tuchel aliiambia Canal Plus.

"[Lakini] anasifa ni wa kipekee ana ubora wa kipekee. Anacheza katika timu nzuri; tulikuwa tayari kutengeneza nafasi nyingi.

"Ni juu yake, Edi [Edinson Cavani] na Angel [Di Maria] kumalizia nafasi."

Mbappe anakuwa mchezaji kinda kuweza kufikisha mabao 50 Ligue 1 na amefunguka kuendeleza makali hayo.

"Ninafanya kazi kila siku kujaribu na kuisaidia timu yangu kwa uwezo wangu wote," alisema. "Ninajaribu fujifurahisha pia. "Soka bado ni kufurahia. Kufunga mabao na kuvunja rekodi ni kitu kinachonisukuma. Mara zote ninafikiri kwamba siku moja mtu fulani anaweza kuja na kufanya vizuri, hivyo daima unapaswa kwenda zaidi ya mipaka yako."

Wakati PSG haikuwapo katika ubora wake kamili, Tuchel aliridhishwa namna kikosi chake kilivyocheza na umuzi kilichofanya, hasa kufuatia mabao mawili ya Mbappe kupatikana ndani ya dakika 21 za mwisho.

"Katika kipindi cha kwanza Nimes ilijaribu kuziba njia, lakini kipindi cha pili tulicheza vizuri sana, na ubora mkubwa," aliongeza.

"Tungeweza kufunga mabao zaidi kwa sababu tulikuwa na nafasi nyingi."

## KWA UFUPI

**LEICESTER YAMTIMUA KAZI PUEL**
Leicester City imemtimua kocha wao, Claude Puel baada ya kuiongoza klabu hiyo kwa miezi 16 tu. City ilichapwa mabao 4-1 nyumbani na Crystal Palace katika mechi ya Ligi Kuu England ambayo ilikuwa ya mwisho kwa Puel, 57, timu hiyo. ***(BBC)***

**ARSENAL YAONGOZA KWA BISSAKA**
Arsenal inaongoza vita ya kumsajili beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, ambaye anathaminishwa na pauni milioni 40. ***(Sun)***

**NEWCASTLE KUVUNJA REKODI**
Newcastle inajiandaa kuvunja rekodi yao ya usajili na imekubali kulipa pauni milioni 51 ili kumsajili straika Mbrazil Joelinton, 22, kutoka kwa Hoffenheim katika majira ya joto. ***(Sport1, via Star)***

**NIGUEZ KUITOBOA MFUKO BRACA**
Barcelona ipo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 95 kwa kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez, 24, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Chelsea. ***(AS)***

**RAKITIC AZIVUTA BAYERN, UTD**
Manchester United na Bayern Munich zinamfuatilia kiungo wa Barcelona na Croatia, Ivan Rakitic, 30. ***(Mundo Deportivo)***

**HART KUTIMKIA MAREKANI**
KIPA wa Burnley na England Joe Hart, 31, atakuwa akijiandaa kutimkia Ligi Kuu Marekani, MLS. ***(Sun)***

**RONDON ANOGEWA NEWCASTLE**
STRAIKA Salomon Rondon, 29, anayeichezea Newcastle kwa mkopo akitokea West Brom, amefunguka kuwa ni mwenye furaha kuendelea kubaki na 'Magpies' hao zaidi ya msimu huu. ***(Newcastle Chronicle)***

**EVERTON YAMCHANGAMKIA MEUNIER**
Everton imefanya mchakato wa kumsajili beki wa Paris St-Germain, Thomas Meunier, 27. (Le10Sport, via Talksport)

**KLOPP KUJAZWA NOTI SOKONI**
MKURUGENZI Mtendaji wa Liverpool, Billy Hogan, amesema fungu la kutosha kwa kocha Jurgen Klopp litakuwapo majira ya kiangazi kwa ajili ya usajili. ***(Liverpool Echo)***

**OVERMARS AITESA ARSENAL**
Arsenal inataka kumrejesha winga wao wa zamani, Marc Overmars kama mkurugenzi wao wa ufundi, lakini klabu yake ya sasa, Ajax inazuia. ***(Mirror)***

**HOLDING KUFUNGWA ARSENAL**
Arsenal itampa ofa ya mkataba mpya beki Rob Holding, 23, baada ya kusumbuliwa na majeraha kwa muda mrefu Desemba mwaka jana. ***(Mirror)***

**MARCELO KUONDOKA MADRID**
BEKI wa pembeni wa kimataifa wa Brazil, Marcelo yupo tayari kuondoka Real Madrid na Juventus inavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Calciomercato)***



## HABARI MICHEZO




Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva (mbele kulia), akiwa katika picha na kikosi cha timu yake ya Difaa Hassan El - Jadida, kilichoivaa Ittihad Tanger ugenini juzi, kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Morocco na kushinda mabao 2-0. Mabao yote yalifungwa na Msuva. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# KVZ, CHIPUKIZI UWANJANI KESHO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya sare kutawala Ligi Kuu Zanzibar juzi, kitimtim hicho kitaendelea kesho, Jumanne kwa kupigwa michezo mitano ambapo Unguja timu ya KVZ itavaana na Chipukizi katika dimba la Mau ze Dong, wakati Uwanja wa Amaan JKU watavaana na Selem View michezo yote ikipigwa saa 10 alasiri.

Kisiwani Pemba itapigwa michezo mitatu kwa Mwenge kupepetana na KMKM Uwanja wa Finya, huku Jamuhuri na Malindi wakivaana Gombani majira ya saa 10 alasiri wakati saa nane mchana kukiwa na kibarua kigumu kwa HardRock kumenyana na Chuoni.

Baada ya mapumziko ya siku tatu, juzi ligi hiyo iliendelea kuchanja mbuga kwa kupigwa michezo mitano katika viwanja tofauti vya Unguja na Pemba ambapo kwa Kisiwani Unguja ilipigwa michezo miwili katika Dimba la Amaan na Uwanja wa Mau ze Dong.

Katika Uwanja wa Amaan, vinara wa ligi hiyo, KVZ walilazimishwa sare tasa na timu ya Selem View ya Pemba ambapo huo ulikuwa mchezo wa tatu katika mzunguko huu wa pili kwa timu hiyo ya Selem.

Mechi ya kwanza Selem walikutana na Zimamoto na kutoka sare ya bao 1-1, wakati ya pili ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya timu ya Jang'ombe Boys, hivyo matokeo hayo yanaifanya kupata kuvuna alama tatu katika michezo mitatu waliyocheza na kufikisha alama 16 wakiwa nafasi ya 14 katika msimo wa ligi hiyo yenye timu 19.

Aidha, katika Uwanja wa Mau ze Dong timu ya Mafunzo ilifanikiwa kuibuka na ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya timu ya New Star bao pekee la timu ya Mafunzo lilipachikwa na mchezaji Mda Homa katika dakika ya 65 na kuifanya mafunzo kufikisha alama 41 na kuendelea kusalia katika nafasi ya sita.

Katika viwanja vya Kisiwani Pemba, timu ya Malindi imefanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya HardRock mchezo uliopigwa Uwanja wa Gombani majira ya saa 10 alasiri, wakati katika dimba hilo majira ya saa nane mchana Mwenge na Chuoni zilitoka sare tasa.

Na katika dimba la Finya, timu ya Mlandege kutoka Unguja imefanikiwa kuichapa Opec kutoka Kisiwani Pemba kwa mabao 2-0 na kwa matokeo hayo imeendelea kubaki nafasi ya tano kwa kufikisha alama 42 huku wapinzani wao hao wakiendelea kusota nafasi ya pili kutoka mkiani wakiwa na alama zake 11.

# Malindi yajiaminisha ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Malindi inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, imesema inamatumaini makubwa ya kunyakuwa Ubingwa wa ligi hiyo kutokana na ubora wa kikosi chake.

Hayo yameelezwa na mmoja wa kiongozi wa timu hiyo ambaye pia ni meneja masoko wa timu ya Malindi, Lageet Khalid Tamim, wakati akizungumza na gazeti hili ambapo alisema anaipa asilimia kubwa timu hiyo kubeba taji hilo msimu huu.

Alisema Malindi inakikosi kizuri na wachezaji wanapambana vya kutosha pindi wapo dimbani, hivyo haoni kinachoweza kuwazuia kutwaa ubingwa wa Zanzibar mwishoni mwa msimu kwa kuwa tayari wanaonyesha maajabu.

Alisema timu hiyo ambayo imejitathmini zaidi kiwango chao katika michuano ya Mapinduzi Cup yaliyomalizika na kupata uzoefu wa kutosha kutoka katika timu walizokutana nazo, mafanikio hayo yatasaidia kufanya vizuri zaidi katika mzunguko huu wa lala salama .

"Kikosi chetu kizuri sana na ninaamini kitafanya makubwa zaidi kwa msimu huu ikiwamo kunyakuwa ubingwa wa Zanzibar jambo ambalo ndio lengo letu,"alisema.

Hata hivyo, alisema timu ya Malindi kwa sasa ipo kisiwani Pemba na inatarajia kushuka dimbani kesho Jumanne kupambana na Jamuhuri ambapo watahitaji alama tatu ambazo ni muhimu katika mzunguko huu.

Malindi hadi sasa ipo nafasi ya tatu nyuma ya Maafande wa JKU lakini timu zote zikiwa na alama 44 zikitofautiana kwa mabao ya kufunga na kufungwa.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | G | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 25 | 19 | 4 | 2 | 42 | 17 | 61 |
| 2.Azam | 25 | 14 | 8 | 3 | 33 | 16 | 50 |
| 3.Simba | 18 | 14 | 3 | 1 | 38 | 6 | 45 |
| 4.Kinondoni MC | 27 | 9 | 13 | 5 | 31 | 18 | 40 |
| 5.Lipuli | 27 | 9 | 11 | 7 | 23 | 21 | 38 |
| 6.Mbao | 27 | 9 | 9 | 9 | 19 | 24 | 36 |
| 7.Alliance | 28 | 9 | 9 | 10 | 23 | 29 | 36 |
| 8.Coastal Union | 26 | 7 | 13 | 6 | 25 | 26 | 34 |
| 9.Mwadui | 28 | 9 | 6 | 13 | 29 | 30 | 33 |
| 10.Stand United | 28 | 9 | 6 | 13 | 27 | 35 | 33 |
| 11.JKT Tanzania | 27 | 7 | 11 | 9 | 15 | 17 | 32 |
| 12.TZ Prisons | 27 | 7 | 11 | 9 | 19 | 22 | 32 |
| 13.Ndanda | 26 | 8 | 8 | 10 | 17 | 27 | 32 |
| 14.Ruvu Shooting | 28 | 7 | 10 | 11 | 21 | 33 | 31 |
| 15.Mbeya City | 25 | 8 | 6 | 11 | 26 | 29 | 30 |
| 16.Kagera Sugar | 26 | 6 | 12 | 8 | 19 | 25 | 30 |
| 17.Mtibwa Sugar | 24 | 8 | 5 | 11 | 21 | 20 | 29 |
| 18.Singida United | 25 | 7 | 8 | 10 | 18 | 24 | 29 |
| 19.Biashara Utd | 26 | 5 | 8 | 13 | 18 | 29 | 23 |
| 20.African Lyon | 27 | 4 | 9 | 14 | 16 | 32 | 21 |

# SMZ yaimwagia Sifa ZAHLIFE

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamisheni ya Utamaduni na Sanaa, imelipongeza Shirikisho la Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu Zanzibar (ZAHLIFE) kwa kuanzisha kikundi cha sanaa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar.

Uzinduzi wa kikundi hicho ulifanyika Kilimani katika Chuo cha Habari Zanzibar na kujumuisha vyuo mbalimbali vya hapa visiwani hapa.

Akizindua kikundi hicho, Kamishina wa Utamaduni na Sanaa Zanzibar, Shamuni Hashim, kwa niaba ya Waziri wa Vijana, Sanaa na Michezo, alisema kitendo cha shirikisho hilo kuzindua kikundi cha sanaa ni mabadiliko makubwa kwenye sekta ya sanaa visiwani Zanzibar.

Aidha, kwa upande mwingine Shamuna amewataka ZAHLIFE ARTS GROUP kushirikiana na wizara hiyo kwa lengo la kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria ikiwamo kusajili kikundi hicho na kuweza kulindwa haki zao za msingi.

Kwa upande wa changamoto ya ajira, alisema kikundi hicho cha ZAHLIFE ARTS GROUP kinaweza kuwatengenezea mazingira vijana hao kuweza kujiajiri badala ya kutegemea ajira kutoka serikalini.

Jumla ya wasanii 40 wamesajiliwa kwenye kikundi hicho cha vyuo vikuu kikijumuisha sanaa za nyimbo, taarabu, mashairi, filamu na maigizo kwa lengo la kuibua vipaji kwa wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar.

# Michezo

Jumatatu Februari 25, 2019

Nipashe




## Mbappe aweka rekodi, atamani kuzivunja zaidi

HABARI UK. 30

HUFUNGI...



Kipa wa Liverpool, Alisson akiokoa hatari dhidi ya Jesse Lingard, kabla ya mshambuliaji huyo wa Manchester United kuumia katika mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford jana na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: DAILY MAIL**

## Yanga yatinga robo fainali FA

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee la dakika ya 82 lililofungwa na Heritier Makambo, limeiwezesha Yanga kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA baada ya kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Namungo FC.

Raia huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alifunga bao hilo kwa kichwa cha kuparaza, baada ya krosi maridadi ya Deus Kaseke aliyeingia dakika ya 59 kuchukua nafasi ya Ibrahim Ajibu.

Haukuwa ushindi rahisi kwa Yanga kwani walipata upinzani mkali kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

Namungo FC ilipoteza nafasi nzuri ya kupata bao dakika ya 60 baada ya mshambuliaji wake, Reliant Lusajo kumpelekea mpira mkononi kipa Mkongo, Klaus Kindoki akiwa kwenye boksi kufuatia pasi ya kutanguliziwa na mtokea benchi, Kelvin John.

Dakika ya 76 Hashim Manyanya naye akafumua shuti kali akiwa umbali wa mita 18, lakini kipa Kindoki ambaye jana alikuwa kwenye ubora wake, alipangua na kutoa nje ikawa kona isiyokuwa na mafanikio kwa wenyeji.

Zahera alilazimika kumpumzisha beki wa kushoto Haji Mwinyi na kumuingia Gardiel Michael.

Na hiyo ni baada ya Mngwali kunusurika kutolewa kwa kadi nyekundu dakika ya 43 alipocheza rafu inayostahili kadi, huku tayari akiwa na kadi nyingine ya njano, lakini mwamuzi Abubakar Mturo alimuacha, hivyo kocha huyo kumtoa haraka.

# AUSSEMS: ZAMU YA LIPULI KUFIA SAMORA

### Asema Simba sasa ni kuvuna tatu tatu kabla ya kuwafuata Waalgeria huku...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Azam FC juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema wapinzani wao wa mchezo unaofuata, Lipuli ya Iringa wajipange kwa kuwa hawatafanya makosa katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Samora kesho.

Aussems aliliambia Nipashe jana kuwa lengo lao ni kuvuna pointi tatu katika kila mchezo, hivyo wanaenda Iringa kupambana kupata matokeo mazuri ugenini.

"Tutakuwa ugenini, najua Lipuli inaisumbua sana Simba, lakini si kwa wakati huu, tunaenda Iringa kuchukua pointi tatu hilo ndio jambo la msingi," alisema Aussems.

Aidha, alisema pamoja na upinzani wanaoutegemea kutoka kwa Lipuli wamejipanga kikamilifu kuhakikisha wanaendeleza kasi yao ya ushindi.

"Unajua mpira ni mchezo wa makosa... ukikosea unaadhibiwa, hatutaki kufanya makosa, nimeongea na wachezaji wangu na kila mmoja ana morali ya kufanya vizuri," alisema Aussems.

Simba inaingia uwanjani Jumanne kumana na Lipuli inayonolewa na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Selemani Matola ikiwa na morali wa kushinda mechi nne mfululizo.

Mabingwa hao watetezi waliichapa Al Ahly bao 1-0 Uwanja wa Taifa kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kabla ya kuibuka na ushindi kama huo dhidi ya watani zao, Yanga katika mechi ya Ligi Kuu.

Baada mechi hiyo, Simba iliichapa African Lyon kwa mabao 3-0 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha na kisha kurejea Uwanja wa Taifa na kuichapa Azam FC 3-1.

Katika mchezo huo wa pili msimu huu kati ya Simba na Lipuli utaamua nani mbabe kufuatia mechi ya mzunguko wa kwanza kutoka sare tasa.

Baada ya mchezo huo, Simba itarejea Dar es Salaam kujiandaa na safari ya Algeria kwa ajili ya mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya JS Saoura

Katika michuano hiyo, Simba inashika nafasi ya pili kwenye Kundi D, ikiwa na pointi sita moja nyuma ya Al Ahly ya Misri, huku JS Saoura ikifuata kwa pointi tano na AS Vita ya DR Congo ikiburuza mkia kwa alama nne.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >